SUPA JACKPOT
TZS. 1,069,861,169
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



**Mke** wa marehemu, ndugu wavutana eneo kuzika mume

UKURASA 4


Nipashe TESA
Teknolojia kidijitali inavyopunguza safari za kwenda ofisi
Kushawishi watoto kujifelisha mitihani kunavyomaliza Pwani
Iringa yawa 'kuzimu' kwa watoto, taifa la kesho lawekwa hatarini
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI
ELIMU
NA MWANDISHI WETU
Ujio madawati jinsia vyuoni uambatane na bidii, si kusubiri fadhili, maksi za bure

UKURASA 11

# Nipashe

Jumanne Januari 24, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0581200
www.ippmedia.com
The Guardian digital
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US

## YALIYOMO

UKURASA WA 4

### CHADEMA YATUMA SALAMU WANAOTAMANI UBUNGE MWAKA 2025



MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Kanda ya Nyasa, Mch. Peter Msigwa ametuma...

UKURASA WA 4

### WANANCHI WAELEZA MACHUNGU KUPAA BEI ZA VYAKULA NCHINI



WAKATI serikali ikiendelea na jitihada za kukabili mfumuko wa bei nchini wafanyabiashara jijini Dar es Salaam...

UKURASA WA 5

### PAC YASHTUKIA RIBA MIRADI YA TANROADS



KAMATI ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) imebaini ucheleweshaji wa malipo ya makandarasi kwenye miradi ya ujenzi...

## Ziara Samia nje kuleta wawekezaji, kampuni 400

UKURASA 2

# Masharti sasa yalegezwa Bima Afya kwa Wote

UKURASA 2

## HUDUMA ZILIZOGUSWA




Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu.

# Lissu kuanza na Mwembe Yanga

UKURASA 3

**MICHEZO** OLIVEIRA: WACHEZAJI SIMBA WAMENIELEWA UK.24

**KATUNI** UK.6



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenista Mhagama, akifurahia jambo na Mama Janeth Magufuli mjane wa Rais Hayati Dk. John Magufuli, baada ya kuwasilisha salamu za Rais Samia Suluhu Hassan, alipoenda kumjulia hali nyumbani kwake jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Masharti yalegezwa Bima Afya kwa Wote

**Na Maulid Mmbaga**

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu, amesema serikali imesikia maoni ya Watanzania na kufanya marekebisho ya Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote kwa kupunguza masharti yatakayomlazimisha mtu kuwa mwanachama.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Ummy alisema muswada wa awali ulifungamanisha huduma muhimu za kijamii tisa ambazo mtu anapokwenda kuziomba, lazima awe amejiunga na bima ya afya lakini baada ya kusikiliza maoni ya wadau nne zimeondolewa na kubakia tano.

Alisema huduma zinazopendekezwa kuondolewa ni utambulisho wa mlipakodi (TIN Number), usajili wa laini za simu, hati za kusafiri, usajili wa wanafunzi wa kidato cha tano na sita na utoaji wa kitambulisho cha taifa.

Zitakazobakia ni leseni ya udereva, bima za vyombo vya moto, leseni za biashara, Visa kwa wageni na usajili wa wanafunzi wa vyuoni.

"Dhana ya ufungamanishaji inalenga kuwezesha utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, kuweka ulazima wa kila mwananchi kuwa na bima ya afya na kuweka msukumo wa kila mwananchi kujiunga na bima ya afya kabla ya kuugua.

"Malengo mengine ya ufungamanishaji huo ni kutekeleza dhana ya kuchangiana gharama za matibabu miongoni mwa wananchi na kuongeza kundi la wananchi wanaonufaika katika mfumo wa bima ya afya," alisema Ummy.

Waziri huyo alisema utekelezaji wa ufungamanishwaji utafanyika kwa awamu kwa makundi ya kimkakati, akibainisha kuwa awamu ya kwanza inatakayoanzia mwaka huu hadi 2026, makundi yatakayofungamanishwa ni pamoja na wageni wanaoingia nchini na wanafunzi wa vyuo vikuu.

Alisema awamu ya pili itaanza 2026 hadi 2028, ikihusisha sekta isiyo rasmi kupitia leseni za biashara, udereva na bima za vyombo vya moto.

Awamu ya tatu kwa mujibu wa waziri huyo, itaanza mwaka 2029 na kuendelea, ikihusisha utekelezaji wa Bima ya Afya kwa Wote kwa ulazima kupitia ufungamanishaji.

"Katika hatua za utekelezaji wa awamu zote, elimu na ubora wa huduma ndiyo msingi wa kuvutia wananchi kujiunga na kuendelea kuhuisha uanachama katika bima ya afya," alisema.

Ummy alitaja mapendekezo mengine ikiwamo kufutwa kwa Sheria ya Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) na CHF iliyoboreshwa na kuanzisha kitita cha Mafao ya Huduma za Msingi cha Jamii, akifafanua kwamba kimefutwa kutokana na upungufu, akikitolea mfano kiwango cha michango kutoendana na gharama halisi za huduma.

Mengine ni uhiari wa wananchi kujiunga na kusababisha wigo mdogo wa wanachama, akibainisha kuwa asilimia sita pekee ya wananchi walijiunga kwa kipindi cha miaka 20 na ufinyu wa huduma katika kitita cha mafao kinachotolewa.

Alibainisha kuwa utaratibu utawekwa kwa wanachama wa CHF kuendelea kupata huduma katika kipindi chote cha mpito na kwamba uzoefu na maboresho vilivyopatikana kutokana na utekelezaji wa CHF vitatumika.

"Maboresho mengine wananchi wasio na uwezo watawezeshwa kupata huduma za afya baada ya kutambuliwa na mamlaka husika, watagharamiwa upatikanaji wa huduma za afya, fedha zitatengwa na Wizara ya Fedha, pia kaya ya watu sita itaundwa na mwanachama mchangiaji, mwenza na wategemezi wasiozidi wanne.

"Pia mifuko ya bima ya afya ya umma na kampuni binafsi za bima ya afya zitafanya tathmini ya uhai na uendelevu kila baada ya miaka mitatu, kumpa mamlaka waziri mwenye dhamana ya masuala ya afya kuboresha mifuko ya bima na kuimairisha usimamizi na udhibiti wa bima, jukumu litakalotekelezwa na Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Bima (TIRA)," alisema Ummy.

Aliongeza kuwa mapendekezo mengine ni kuwa na kitita cha mafao ya huduma muhimu ambacho kila skimu ya bima ya afya italazimika kukitoa na kitakuwa ni haki ya kila mwanachama.

Alisema kitita cha mafao cha huduma muhimu kitajumuisha ada ya uandikishaji na kumwona daktari, gharama za vipimo, dawa aina zote, upasuaji mdogo na mkubwa, kulazwa, huduma ya afya ya kinywa na meno, matibabu ya macho, vifaa saidizi na huduma za mazoezi ya viungo.

**MANUFAA TARAJIWA**

Mwenyekiti wa Kikosi Kazi cha Bima ya Afya kwa Wote, Bernard Konga, alisema baada ya maboresho hayo kupitishwa, kundi kubwa la wananchi litakuwa na uhakika wa kupata huduma za matibabu bila kikwazo cha fedha, uboreshaji wa huduma kwenye vituo vya kutolea huduma za afya kwa umma, ikiwa ni pamoja na kuimarika kwa upatikanaji wa dawa, vifaa na vifaa tiba.

Alisema yatasaidia pia katika uhimilivu na ustahimilivu wa mfuko katika kutoa huduma, kuimarika kwa usimamizi na udhibiti katika utoaji wa huduma za bima zitolewazo na mifuko na kampuni binafsi za bima hiyo, kuboreshwa kwa vitita vya mafao vinavyotolewa na mifuko husika na kuimarisha hali ya kipato kwa wananchi.

## Ziara za Samia nje kuleta wawekezaji, kampuni 400

**Na Mwandishi Wetu**

UMOJA wa Ulaya umesema ziara ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwenye nchi hizo zimekuwa na matokeo chanya baada ya zaidi ya wafanyabiashara, kampuni na wawekezaji 400 kutoka nchi 27 za bara hilo kuja nchini kwenye kongamano la kibiashara litakalofanyika Februari 23 na 24, jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Balozi wa Umoja wa Ulaya, Manfredo Fanti, alisema kongamano hilo litawaleta pamoja watu zaidi ya 600 kutoka nchi mbalimbali duniani wakiwa na lengo la kuziona fursa na kuamua kuwekeza nchini.

Alisema mafanikio ya kongamano hilo ni kutokana na Rais Samia alipotembelea baadhi ya nchi za Ulaya na kukutana na wawekezaji, kampuni na wafanyabiashara aliowaomba kuja nchini kuendeleza majukumu yao.

Alisema EU inaridhishwa na hatua mbalimbali zinazochukuliwa ikiwamo kuhakikisha mazingira rafiki kwa wawekezaji na sasa wanaona fursa na umuhimu wa sekta mbalimbali ambazo kundi hilo linaweza kuwekeza.

Alisema Rais Dk. Samia atafungua kongamano hilo na kufungwa na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi.

Kongamano hilo linatarajiwa kuwa na mada mbalimbali kama kupata masoko ya mazao ya kilimo Ulaya, Nishati mbadala, miradi ya benki, viwanda, uunganisho wa vifaa, ujenzi, digitali, usafiri na usafirishaji, ukuzaji wa ujuzi, fedha, namna Tanzania inaweza kukua, uwekezaji Bara na Visiwani.

"Tunawaleta nchini wakutane na sekta binafsi ya Tanzania, Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), wanasiasa na viongozi wa juu wa serikali ambao watawaeleza na kuwaonyesha fursa zilizoko, tunaamini katika majadiliano na mawasilisho ya siku mbili wataona ni maeneo yapi wanaweza kuwekeza," alisema.

Balozi Fanti alisema pia kutakuwa na hafla ya kusaini makubaliano na mikataba mbalimbali baada ya kufikia mwafaka baina ya pande zote.

Naye Mkuu wa Ushirikiano wa EU, Cedric Merel, alisema wameona kuna hatua kubwa imepigwa kwenye sekta mbalimbali nchini na kuna mabadiliko makubwa ya kisera na sheria ambayo yanavutia wawekezaji kuja nchini.

"Tumeona kupitia kongamano hili itakuwa ni sehemu sahihi ya kuimarisha ushirikiano baina ya EU na Tanzania, kuna fursa nyingi tumeziona na tunaamini kampuni kubwa na wawekezaji wakubwa watazïona na kuzitumia, tayari tunajihusisha kwenye sekta mbalimbali nchini na tutaendelea kufanya hivyo," alisema.

Alisema Tanzania ni nchi inayokuwa kwa kasi kiuchumi huku ikitoa nafasi kwa vijana na wanawake ambako kote huko EU imeonyesha nia na kuna miradi inayofadhiliwa inaendelea.

Naye Mkurugenzi wa Utafiti na Mipango wa Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), Maftah Bunini, alisema kongamano hilo ni muhimu kwa maendeleo ya nchi kutokana na soko la EU Watanzania hawajalifikia vizuri.

"EU kuna soko kubwa ambalo bado hatujalifikia vizuri, sasa watakuja watu muhimu 400 kutoka nchi 27 tutalielewa vyema soko hilo muhimu kibiashara na kuona fursa za kuuza bidhaa na mazao, lakini na wao wataona fursa za kuwekeza nchini," alisema.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, kongamano hilo ni jitihada za serikali kufungua fursa na mazingira ya biashara kwa wananchi wake ambao watanufaika mmoja mmoja na taifa kwa ujumla kutokana na wawekezaji na wataalamu kutoka sekta zote muhimu kuja ikiwamo teknolojia.

"Hizi ni jitihada za serikali kwa sasa kuvutia wawekezaji na wafanyabiashara duniani kuwekeza kwenye sekta zetu muhimu ambazo ni nishati mbadala, madini ya kimkakati, kilimo endelevu. Tunatarajia kusaini makubaliano na mkataba wenye maslahi kwa umma ambayo italeta fursa kwa vijana na kuboresha kipato cha watu," alisema.



Mtafiti wa Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI), Makrina Komba, akimuuliza maswali, Mwajuma Kidawa aliyefika katika Hospitali ya Rufani Mnazi Mmoja Zanzibar kwa ajili ya kupata huduma ya upimaji na matibabu ya moyo yanayofanyika katika hospitali hiyo. JKCI kwa kushirikiana na Hospitali ya Mnazi Mmoja Zanzibar wanafanya kambi maalum ya matibabu ya moyo ya siku tano kwa watoto na watu wazima. **PICHA: JKCI**

# Lissu kuanza na Mwembe Yanga

**Na Elizabeth Zaya**



KAMATI maalumu inayoratibu mapokezi ya Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, iliyopewa jina la 'Lissu Home Coming', imewaomba wafuasi wa chama hicho na wakazi wa Jiji la Dar es Salaam kujitokeza kwa wingi kesho kumpokea kiongozi huyo.

Kwa mujibu wa Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Mch. Peter Msigwa, Lissu atawasili kesho saa 7:30 mchana kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere(JNIA).

Mch. Msigwa alisema kuwa baada ya kuwasili, Lissu atakwenda moja kwa moja kwenye viwanja wa Mwembe Yanga, Temeke kufanya mkutano wa hadhara kuzungumza na Watanzania.

"Mimi ni mwenyekiti wa kamati ndogo inayotokana na Kamati Kuu ya chama, maarufu Lissu Home Coming, na ndio maana niliondoka Mwanza kuja hapa kwa sababu hiyo ya kushughulikia mapokezi yake kwa kushirikiana na CHADEMA Kanda ya Pwani.

"Na baadhi waliopo katika kamati hii ni pamoja na Mwenyekiti wa CHADEMA Kanda ya Pwani, Baraka Mwago, Grace Kiwelu na mwingine wa Zanzibar.

"Kwa hiyo, niwakaribishe wakazi wa Dar es Salaam tukampokee shujaa wetu uwanja wa ndege na kisha twende Temeke tukamsikilize Lissu maana anafundisha, anaelimisha na tutapata mambo mengi kutoka kwake," Mch. Msigwa alisema.

Lissu aliondoka nchini Septemba 2017 kwenda Nairobi, Kenya kwa matibabu baada ya kushambuliwa kwa risasi kwenye makazi yake Area D jijini Dodoma muda mfupi baada ya kutoka bungeni.

Baada ya shambulio, alikimbizwa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma kwa matibabu na baadaye alisafirishwa kwenda Nairobi, Kenya kwa matibabu kisha kusafirishwa kwenda Ubelgiji ambako aliendelea na matibabu hadi aliporejea nchini kwa mara ya kwanza Julai mwaka 2020, akashiriki Uchaguzi Mkuu akiwania nafasi ya urais kwa tiketi ya CHADEMA.

Novemba 10, 2020, Lissu aliondoka tena nchini, akisindikizwa hadi uwanja wa ndege na Balozi wa Ujerumani kwenda Ubelgiji baada ya kumalizika kwa uchaguzi mkuu, akidai usalama wa maisha yake ulikuwa shakani.

Januari 13, mwaka huu, Lissu alizungumza na Watanzania kupitia mitandao ya kijamii na kueleza kusudio lake la kurudi nchini Januari 25. Wiki iliyopita, Mkurugenzi wa Itikadi, Mawasiliano na Mambo ya Nje wa CHADEMA, John Mrema, alisema maandalizi ya kurejea kwa viongozi wote wa chama hicho ambao ni wakimbizi wa kisiasa, yanafanyika kwa hatua mbalimbali.

Alitaja viongozi wengine wanaojiandaa kurejea nchini mbali na Lissu kuwa ni pamoja na Godbless Lema ambaye alikuwa Mbunge wa Arusha Mjini.

# Tanzania yaunga mkono mkakati wa kijinsia IMF

**Na Benny Mwaipaja**

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, amesema Tanzania inaunga mkono mpango ulioanzishwa na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) la kuingiza masuala ya kijinsia kwenye utekelezaji wa mipango yake ya maendeleo.

Dk. Nchemba ametoa kauli hiyo wakati akifungua mkutano wa majadiliano kuhusu mkakati wa shirika hilo wa kuingiza masuala ya kijinsia kwenye mipango yake, uliofanyika jijini Dar es Salaam na kuwashirikisha wadau mbalimbali kutoka ndani na nje ya nchi.

Alisema Serikali ya Tanzania itaendelea kutilia mkazo masuala ya kijinsia kwa kuwekeza rasilimali fedha katika kuboresha afya ya mama na mtoto, utoaji elimu bila ada na kuwawezesha wanawake kiuchumi.

Dk. Nchemba aliiomba Jumuiya ya Kimataifa kuendelea kushirikiana na serikali katika kufanikisha masuala hayo na kusifu ushirikiano uliopo kati ya Tanzania na IMF na ushirikiano huo umelenga katika maeneo matatu ikiwamo kuelekeza bajeti kubwa kwenye maendeleo ya watu kwa kuboresha makusanyo ya ndani kupitia kodi, kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara na kuimarisha usimamizi na matumizi ya fedha za umma.

Alisema maendeleo ya kijamii katika sekta ya fedha na kuimarika kwa uchumi katika miaka ya hivi karibuni kumechangia kuongezeka miaka ya kuishi kwa Watanzania, kupungua kwa vifo watoto chini ya umri wa miaka mitano, kupungua kwa udumavu pamoja na kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi wa jinsi zote wanaojiunga na masomo kwenye shule za msingi.

Akizungumza kwenye mkutano huo, Mkurugenzi wa Kituo cha Shirika la Fedha la Kimataifa Mashariki (AFRITAC), Li Xiangming, alisema uamuzi wa Shirika lake kuingiza masuala ya kijinsia kwenye mipango yake imelenga kujenga jamii yenye usawa na kuwawezesha wanawake kushiriki kujenga uchumi na kupata maendeleo endelevu.

Alitaja baadhi ya maeneo yatakayotiliwa mkazo zaidi katika mkakati huo kuwa ni pamoja na kuwawezesha wanawake kiuchumi, kumiliki ardhi, kupata elimu bora na kupiga vita aina zote za ukatili wa kijinsia zinazokwamisha maendeleo ya mwanamke na mtoto.

Mwakilishi Mkazi na Mratibu wa Shirika la Umoja wa Mataifa, Zlatan Milisic, aliipongeza Tanzania kwa kusimamia uchumi wake vizuri licha ya kuwapo kwa changamoto za UVIKO-19 pamoja na vita vinavyoendelea baina ya Urusi na Ukraine.

Aliahidi kuwa IMF kwa kushirikiana na Umoja wa Mataifa wataongeza jitihada katika kuiwezesha Tanzania kufikia malengo yake ya maendeleo ya milenia katika masuala mbalimbali ikiwamo kuwawezesha wanawake kiuchumi ili kujenga jamii iliyo bora na jumuishi kiuchumi na kijamii.

Mkutano huo wa majadiliano kuhusu mkakati wa IMF wa kuingiza masuala ya kijinsia katika mipango yake umehudhuriwa na wadau mbalimbali kutoka ndani na nje ya nchi.

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

**KURUDIWA TANGAZO**

Tangazo la awali la tarehe 18.01.23 lilikuwa na makosa ya tarehe ya mwisho kutuma maombi, tarehe sahihi ni 02.02.2023

BBN Limited TZA

**OMBI LA KUONESHA MASLAHI KWA UTOAJI WA HUDUMA (3rd Party Services) ZA UCHOMELEAJI, UPAKAJI NA NDT**

**ETJ-BB-PR-EI-GEN-GE-0017 / ETJ-BB-PR-EI-GEN-GE-0018**

BESIX Ballast Nedam Limited, inayotekeleza Huduma za Awali za mradi wa Gati na Kituo cha Upakiaji katika Ghuba ya Tanga kwa ajili ya Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP), inakaribisha Makampuni ya kitaalamu kueleza nia yao kwa:

- **Ukaguzi wa kuchomelea chuma, Upakaji na NDT, Ukaguzi wa Utaratibu wa kuchomelea, Uhitimu wa Welder, Mafunzo na Udhibitishaji wa Wakaguzi wa Mradi na vifaa vya kufanyia Destructive Testing.**

Jamhuri ya Uganda, Kampuni ya Taifa ya Mafuta ya Uganda (UNOC), Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na/au Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), pamoja na makampuni mengine ya kimataifa ya mafuta yanashiriki katika utekelezaji wa Mradi wa EACOP.

Uendelezaji wa Mradi wa EACOP unahusisha uhandisi, ujenzi, uendeshaji na matengenezo ya bomba la kusafirisha mafuta ghafi linalovuka Uganda na Tanzania ikijumuisha. Gati yenye Kituo cha Kupakia Mafuta kwa Meli za Mafuta, karibu na Tanga nchini Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI YA WIGO WA VIFAA / HUDUMA:**

* Mkaguzi wa kuchomelea (1) - Kiwango cha chini cha CSWIP daraja la 1 au cheti sawa
* Mkaguzi wa Mipako (1) - Kiwango cha chini BGAS/CSWIP Daraja la II, NACE daraja la II, SSPC na ICORR daraja la II
* Mkaguzi wa NDT (1) - Daraja la II (UT, RT, MT, PT) kulingana na ISO EN 9712
* Sifa za Mchomeleaji (Welder) kulingana na EN 9606-1 na ASME BPVC Sehemu ya IX
* Sifa za Utaratibu wa Kuchomelea kulingana na EN 1090 na ASME B31.3
* Mafunzo na uidhinishaji wa wafanyikazi wa mkandarasi wakati wowote inapohitajika kwa uchomeleaji, upakaji rangi maalumu kwenye chuma na NDT.
* Upimaji wa Vifaa vya Mradi kulingana na viwango vya Mradi.

**KIWANGO CHA MAHITAJI:**

Kampuni zinazoonyesha nia yao zinaalikwa kuandika ombi lao kwa kuambatanisha:

- Wasifu wa kampuni wenye uthibitisho wa uwezo wa kutosha wa kifedha na rasilimali za kutosha na zenye uwezo kusimamia kandarasi.
- Orodha ya tajriba iliyo na historia ya ugavi ya kazi husika / rekodi inayoonyesha uzoefu usiopungua miaka mitano (5) katika utekelezaji wa huduma zinazofanana za huduma za uchomeleaji na mipako kulingana na viwango vya kimataifa vinavyojulikana katika biashara ya Mafuta na Gesi au soko linalolinganishwa.
- Orodha ya kina ya wakaguzi waliohitimu na kuithinishwa,
- Orodha ya vifaa vya NDT na mipako,
- CV za Wakaguzi,
- Sera ya Ubora wa Kampuni na mipango ya Afya, Mazingira na Usalama Eneo la Kazi na uthibitisho: ISO 9001:2015, ISO 14001:2015
- Rasimu/Sampuli ya ripoti ya ripoti katika umbizo la pdf,
- Kuzingatia kanuni za mafuta ya petroli (Local Content) ya 2017 na ufafanuzi wa kampuni ya ndani kwa Tanzania,
- Uthibitisho wa usajili/maombi kwa hifadhidata ya Watoa Huduma kwa Wasambazaji wa Ndani (LSSP) wakati wa kuwasilisha jibu kwa usemi huu wa maslahi unapendekezwa sana.

Makampuni yanayovutiwa ambayo yanakidhi mahitaji na yana uwezo wa kutoa huduma, yanapaswa kueleza nia yao kwa kutuma pamoja na hati zilizoorodheshwa hapo juu barua pepe kwa **procurement@bbnltd.co.tz (Ukubwa wa Barua pepe na viambatanishi: 20 MBs & Nyaraka zote lazima ziwasilishwe kwa lugha ya Kiingereza)** mnamo au kabla ya tarehe **02 February 2023, 12:00 jioni** Saa za Tanzania,

Makampuni yanayokidhi kwa kuridhisha mahitaji ya chini zaidi yaliyo hapo juu yatatathminiwa na yakichaguliwa yataalikwa, kulingana na saini ya Makubaliano ya Kutofichua (NDA), ili kushiriki katika mchakato wa zabuni.

**Kumbuka :** Kampuni zilizohitimu awali pekee ndizo zitapokea mwaliko wa kuwasilisha zabuni yao ili kuendeleza mchakato wa Wito wa Zabuni.

17232302

# Wananchi waeleza machungu kupaa kwa bei za vyakula

**Na Jenifer Gilla**

WAKATI serikali ikiendelea na jitihada za kukabili mfumuko wa bei nchini wafanyabiashara jijini Dar es Salaam wamelalamikia kuendelea kupanda gharama za bidhaa hasa mchele na maharage kunavyoathiri shughuli zao na kuwarudisha nyuma kimaendeleo.

Wameiomba serikali kuingilia kati kuwanusuru na hali hiyo kutokana na baadhi yao kulazimika kufunga biashara kuepuka hasara.

Wiki iliyopita Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha na Mipango, Lawrence Mafuru, alisema, serikali inaendelea kuchukua hatua kuhakikisha upungufu wa chakula na mfumuko wa bei ya bidhaa hauathiri wananchi.

Aliyataja maeneo yatakayosaidia nchi kujiimarisha kiuchumi, kuwa ni sekta ya utalii, kilimo, maliasili, gesi asilia na usafirishaji kutokana na eneo la kijiografia Tanzania ilipo.

Alisema maliasili hizo zikifanikiwa kutumika vizuri nchi itakuwa imejikomboa kwa kupata unafuu wa mfumuko wa bei ambao umeiathiri dunia kwa sasa.

Akizungumzia kilimo, Mafuru alisema mikakati inapowekwa vizuri uzalishaji wa chakula utaongezeka na kutoa fursa ya kuuzwa ndani na nje ya nchi na pia kuwa na akiba ya kutosha.

Mmoja wa wafanyabiashara wa mchele Tabata sokoni, Alphonce John, alisema bidhaa hiyo inapanda kila mara na kuathiri mauzo yake na wateja kupungua.

"Kwa kipindi cha mwezi mmoja mchele umepanda mara tatu na kunilazimu kupandisha kutoka Sh. 3,000 hadi Sh. 3,800 kwa mchele huu wa super, matokeo yake nimepoteza karibuni asilimia 50 ya wateja wangu," alilalamika.

Alphonce alisema mauzo yamepungua kutoka kuuza gunia la kilo 100 kwa wiki na hadi wiki mbili na hauzi wote.

Mamalishe Amina Mselemo, alisema aliacha kuuza wali baada ya mauzo yake kuathirika kutokana na kupaa kwa bei hizo, wakati anaanza kilo ya mchele alikuwa ananunua Sh. 2,500 sasa imefika Sh. 3,500.

"Wakati naanza biashara kilo tano za mchele na kilo mbili za maharage nikiuza napata faida ya Sh. 15,000, ikawa inapungua kadiri nafaka hizi zinavyopanda. Wiki iliyopita nikapata faida Sh. 3,000 nikaona niachane nayo," alisema.

Dotto Salim, mpishi wa chapati na maharage katika soko la Temeke, alisema amelazimika kupandisha bakuli moja kutoka Sh. 500 hadi 700, ili kufidia gharama zilizoongezeka na kusababisha wateja wake kumkimbia.

Sadik Abdallah, kutoka Ilala alisema ameamua kuchanganya mchele na unga wa mahindi kupika vitumbua ili kuepuka gharama.

"Imebidi nijiongeze ili nisipandishe bei ya vitumbua nikapoteza wateja, kwa kawaida unga wa mchele unatakiwa uwe mwingi na wa ugali kidogo, lakini mimi naweka nusu kwa nusu na ninaongeza na unga wa ngano kidogo na vinatoka vizuri tu huwezi kuona tofauti," alisema Angela.

**SABABU KUPAA BEI**

Mfanyabiashara wa maharage ya jumla katika Soko la Tandika, Shekhe Mbwana alisema, upungufu wa mvua, umedhorotesha shughuli za kilimo mwaka jana na kuathiri upatikanaji wa nafaka ya kutosha.

Alitoa mfano wa baadhi ya mikoa vinara wa kilimo cha maharage ambayo kwa sasa ina upungufu wa nafaka hiyo ikiwamo Arusha, Sumbawanga na Morogoro na kutegemea mikoa ya Kagera na Njombe.

"Kwa sasa bei ya jumla ya maharage tunauza kuanzia Sh. 2,800 aina ya kombati na hii imeshuka tulikuwa tunauza Sh. 3,300, na bei ya juu ni Sh. 3,500 haya ni maharage ya njano ambayo upatikanaji wake ni shida ndiyo maana bei ipo juu," alifafanua.

Aidha, mfanyabiashara wa mchele kwa jumla katika soko Temeke, George Mashaka, alitaja sababu nyingine ni wakulima wa ndani kuangalia zaidi masoko ya nje ya nchi kwa ajili ya maslahi yao.

Kwa mujibu wa Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara bei za jumla za mazao makuu ya chakula nchini kwa kilo 100 mkoani Dar es Salaam hadi kufikia Januari 16, mwaka huu, mahindi ni Sh. 105,000, mchele Sh. 280,000 hadi 300,000, na maharage Sh. 300,000 hadi 340,000 na viazi mviringo Sh. 110,000 hadi 130,000.




Meneja wa Tanzania Commercial Bank (TCB) Tawi la Mbagala, Edward Mwoleka (kushoto), akikabidhi msaada wa mifuko 100 ya saruji kwa Diwani wa Kata ya Kiburugwa wilayani Temeke, Fatuma Michael, iliyotolewa na benki hiyo kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa kituo kipya cha polisi cha kata hiyo jijini Dar es Salaam jana. Wengine ni Meneja wa Mawasiliano na Uhusiano wa TCB, Gloria Mutta na Ofisa wa TCB, Adam Lameck. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# CHADEMA yatuma salamu wanaotamani ubunge 2025

**Na Elizabeth Zaya**

MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Kanda ya Nyasa, Mch. Peter Msigwa, ametuma salamu kwa wenye mpango wa kuwania ubunge katika Uchaguzi Mkuu ujao, akionya kuwa wasiende kwa mazoea na kwa taswira ya uchaguzi wa mwaka 2020.

Amesema uchaguzi ujao utakuwa na ushindani na hakutakuwa na alichokiita mbeleko, hivyo wenye nia wajipange vizuri.

Mch. Msigwa aliyasema hayo alipohojiwa na moja ya vituo vya televisheni mkoani Dar es Salaam.

Alidai kuwa uchaguzi wa mwaka 2020 haukuwa na ushindani kwa sababu ulitawaliwa na kubebwa badala ya kushindana.

"Katika uchaguzi uliopita, mimi ni mmoja wa wagombea ubunge ambao walifanya kampeni nzuri kwa ubora, nilikuwa na ajenda na timu bora lakini yalitokea yaliyotokea, kwa uchaguzi ujao ambao Rais Samia Suluhu Hassan ameonyesha kwamba kutakuwa na uchaguzi wa haki, wanaotaka kushindana wajipange, kwa sababu kutakuwa na ushindani ambao ni wa uhakika, hakutakuwa na kubebwa.

"Niwasikitikie wale ambao wanataka kuitwa washindi wakati hawakushindana, ili uitwe mshindi ni lazima ushindane. Wale wabunge ambao wanajua hawakushinda katika majimbo yao, iwe ndani ya vyama vyao ambao wengi walichukuliwa watu wa tano, na hata tulivyokuja kwenye uchaguzi mkuu hawakushinda, wajiopange vizuri sana, kwanza hawana uhusiano mzuri na wananchi.

"Unajua kama unafahamu kwamba hukuchaguliwa, hata kuweka tu mkutano huwezi, anakusikiliza nani? Kwa hiyo, wanatakiwa wajipange kwa sababu tunakuja kivingine kabisa na hoja za msingi, hoja shawishi, fundishi na fikirishi kwa ajili ya kujenga taifa letu. Safari hii mbeleko haipo tena," alisema.

Kuhusu makundi yanayojiita chawa kwenye vyama vya siasa, Mch. Msigwa alisema hao ndiyo wanaharibu taswira ya tasnia hiyo nchini.

# Mke wa marehemu, ndugu wavutana eneo la kumzika mume

**Na Mwandishi Wetu**

FAMILIA ya aliyekuwa mfanyakazi wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Henry Massawe, imeingia kwenye mvutano wa wapi uzikwe mwili wa mpendwa wao huyo kwa kile kilichodaiwa wosia wa marehemu.

Mke wa marehemu, Janeth Ikuyumba anataka mwili wa mumewe ukazikwe Moshi mkoani Kilimanjaro alikozaliwa wakati ndugu wa marehemu wanataka uzikwe nyumbani kwake Kiharaka, Bagamoyo mkoani Pwani.

Licha ya kaburi kuchimbwa nyumbani kwake Kiharaka, mwili wa kijana huyo aliyefariki dunia Januari 16 mwaka huu kwenye Hospitali ya Regency jijini Dar es Salaam, haujazikwa.

Mmoja wa mashuhuda wa mgogoro huo ambaye aliomba hifadhi ya jina lake, alidai kuwa kabla ya kifo chake, kijana huyo aliyekuwa Ofisa Viwango TBS, aliomba akifariki dunia, azikwe nyumbani kwake. "Ijumaa (iliyopita), tuliandaa kaburi ili tumzike Henry lakini mvutano ulizidi kiasi kwamba tulishindwa kuzika. Mke anadai kwamba anataka kuipangisha nyumba, hivyo kukiwa na kaburi, itamkosesha biashara," alidai shuhuda huyo.

Aliendelea kudai kuwa mke amekataa kumzika mumewe kwenye eneo alilochagua kwa kuwa "hata akitaka kuuza nyumba, itakuwa ngumu kuuzika."

Alisema kuwa Masawe ameacha mtoto mmoja wa kiume anayekadiriwa kuwa na umri wa miaka miwili.

NIPASHE ilipomtafuta mke wa marehemu, Janeth Ikuyumba kuhusu suala hilo, alikataa kulizungumzia kwa madai kwamba aliyetoa taarifa ya mvutano huo, anayo maelezo ya kutosha.

"Kamuulize huyo aliyekwambia hizi habari, akufafanulie zaidi maana inaonekana anajua kila kitu, mimi sina cha kusema," alisema.

NIPASHE ilimtafuta dada wa marehemu, Sesilia Massawe ambaye alithibitisha kuwapo mvutano huo. Hata hivyo, alishindwa kutoa ufafanuzi zaidi kwa maelezo kuwa yuko kikaoni na kwa zaidi ya saa tatu alikuwa kikaoni na kila akipigiwa alijibu kuwa hawezi kuongea kwa kuwa kikao kilikuwa hakijamalizika.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Kiharaka Magengeni, Simon Kilian alithibitisha kuwapo mvutano huo, lakini alikataa kutoa ufafanuzi kwa njia ya simu.

Jirani wa familia hiyo, Fatuma Chombo, alidai: "Tumeishi na Henry vizuri sana, alikuwa anasalimia mkubwa hadi mdogo, kaburi limeshachimbwa halafu tunaambiwa hatazikwa Kiharaka, tupo hapa hadi azikwe hapa.

"Tunasikia mke anataka asafirishwe lakini ndugu wa mume wanataka azikwe hapa, jana (juzi) tulikuwa hapa tukatangaziwa anazikwa leo (jana), cha ajabu tumefika hapa tunaambiwa hazikwi hapa na kaburi limechimbwa."

Alidai kuwa awali waliambiwa hawawezi kuchimba kaburi hadi kibali kipatikane na walitafuta kibali kikapatikana kwa viongozi wote na kuruhusiwa kuchimba kaburi tangu juzi.

Alidai kuwa kijana huyo alitakiwa kuzikwa Januari 20, mwaka huu, lakini hadi jana mwili ulikuwa haujafika nyumbani.

## Washtakiwa kesi ya kobe wakwama kufika mahakamani

**Na Grace Gurisha**

ASKARI wawili wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi Tanzania (JWTZ) na washtakiwa wengine sita wanaotuhumiwa kukutwa na kobe 116, wameshindwa kufikishwa mahakamani kusomewa masharti ya dhamana kutokana na changamoto ya usafiri wa magari ya Magereza.

Washtakiwa hao ni mfanyabiashara Josephat Moyo (52), mkazi wa Tabata; Deogratius Lugeng'a (40); MT 88046 Sajenti Cosmas Ndomba kutoka JWTZ na Mfanyabiashara Hamza Abdalah (52).

Wengine ni MT 118102 Kassim Abdalah (35); Nkanamuli Ngaza (52), mlinzi wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA) Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere na wakulima wawili kutoka mkoani Dodoma ambao ni Stephano Chedego (51) na Mwaluko Mgomole.

Washtakiwa hao walitakiwa kufikishwa mahakamani jana mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Rhoda Ngimilanga wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam kwa ajili ya kusomewa masharti ya dhamana.

Kutokana na changamoto hiyo ya usafiri wa Magereza, mahabusu hao walishindwa kufikishwa mbele ya Hakimu Ngimilanga, hivyo masharti yalisomwa mbele ya mawakili wa washtakiwa hao.

Hakimu Ngimilanga alisema ili washtakiwa wawe nje kwa dhamana, wanatakiwa kila mmoja awe na wadhamini wawili ambao ni wakazi wa Dar es Salaam ambao watatakiwa kutia saini bondi ya Sh. milioni tano.

Alisema wadhamini hao pia wanatakiwa kuwa na barua za utambulisho pamoja na kitambulisho cha NIDA au cha mpigakura.

Awali Wakili wa Serikali, Adolf Verandumu, alidai kesi imeitwa kwa ajili ya washtakiwa kusomewa masharti ya dhamana japo hawakuwapo mahakamani lakini wawakilishi wao walikuwapo.

Hata hivyo, Wakili wa washtakiwa hao, Nehemiah Nkoko, aliomba kesi hiyo irudishwe leo ili kuwapa nafasi kukamilisha utaratibu wa washtakiwa kufika mahakamani ili watimize masharti ya dhamana.

Alidai kuwa washtakiwa hawajaletwa mahakamani kwa sababu ya changamoto ya usafirishaji, hivyo anaomba ahirisho hilo la kesi.

"Hapana, hata nikiwaambia kesi leo mtaniambia hivyo hivyo kuwa washtakiwa hawajaletwa kwa sababu ya changamoto ya usafiri, kwa hiyo kesi ipangiwe tarehe nyingine," alisema Hakimu Ngimilanga alipojibu hoja hiyo.

Kesi hiyo iliahirishwa hadi Januari 30, mwaka huu kwa ajili ya washtakiwa kutimiza masharti ya dhamana.

Ilidaiwa mahakamani huko kuwa kati ya Januari hadi Julai 3, 2022, jijini Dar es Salaam, washtakiwa hao waliendesha genge la uhalifu.

Ilidaiwa kuwa waliendesha genge la uhalifu kwa kununua, kukusanya, kusafirisha, kununua na kuuza nyara za serikali ambayo ni kobe 116 wenye thamani ya dola za Marekani 8,120 sawa na Sh. 18,935,840.

Ilidaiwa kuwa katika shtaka la pili, katika tarehe hizo, ndani ya Mkoa wa Dar es Salaam, washtakiwa hao kwa pamoja walijihusisha na nyara hizo kwa kununua na kuziuza bila kuwa na kibali kutoka kwa Mkurugenzi wa Wanyamapori.

# PAC yashtukia riba miradi ya TANROADS

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) imebaini ucheleweshaji wa malipo ya makandarasi kwenye miradi ya ujenzi iliyoko chini ya Wakala wa Barabara (TANROADS) na kusababisha riba zinazoigharimu serikali.

Kutokana na hali hiyo, kamati imeagiza Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kufanya uchunguzi kubaini anayehusika na ucheleweshaji huo.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Naghenjwa Kaboyoka, alibainisha hayo jana baada ya kukutana na Ofisa Masuhuli wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Ujenzi) na Mtendaji Mkuu wa TANROADS kupitia ripoti ya ukaguzi ya CAG kuhusu ujenzi wa daraja la Busisi mkoani Mwanza.

Alisema wamepitia ripoti hiyo kuangalia masuala ya kiufundi ya daraja hilo na kubaini kuna ucheleweshaji wa malipo hayo unaoigharimu serikali kutokana na kudaiwa riba ya takribani Sh. bilioni mbili na makandarasi wa Busisi.

Mwenyekiti huyo alisema mbali na daraja hilo, kuna miradi mingine ambayo makandarasi wanadai fedha za kucheleweshewa malipo na kusababisha hasara ya mabilioni ya shilingi za walipakodi.

"Ucheleweshaji huu unaigharimu serikali fedha nyingi sana kwa kuwa hazipo kwenye mpango wala kwa kazi ile inayofanywa, matokeo yake fedha zilizotakiwa kwenda kwenye maendeleo na kufanya kazi za sehemu nyingine zinakwenda kulipia ucheleweshaji wa kumlipa mhandisi mwelekezi kutokana na ucheleweshaji ambao tunaamini kama TANROADS wangesimama vizuri yasingekuwa haya. "Ukiangalia fedha zinazotolewa Sh. bilioni mbili zingekwenda kufanya kazi sehemu nyingine kwenye vituo vya afya, elimu tuna shida kubwa sana, tatizo hadi leo ukiwauliza wanasema Hazina ndio wanachelewesha kuwapa fedha, tunataka CAG ahakiki.

"Hati mpaka inatolewa na kufikia malipo hapo katikati nani anachelewesha? Maana ukisema Hazina wanachelewesha fedha, tatizo linazidi kuwa kubwa na linakuwa halipo kwenye uwezo wao na kama halipo ina maana matatizo yataendelea mwaka hadi mwaka kutoka mradi mmoja hadi mwingine.

"Matokeo yake ni kwamba nchi yetu haipaswi kuwa na mipango ambayo hatuwezi kutekeleza kwa wakati tunakuwa na mikataba ambayo hatuwezi kutekeleza, matokeo yake tunaishia kulipa riba kubwa, hii riba kwa mkandarasi ni faida kwake na kwa mlipakodi ni hasara," alionya.

Kaboyoka alisema hilo ni tatizo kubwa linaloipa shida kamati hiyo hasa kwenye miradi inayosimamiwa na TANROADS.

Alisema ni vyema serikali ikaangalia mipango ya kuwa na miradi ambayo ina uwezo wa kuwalipa makandarasi kwa wakati na kuepukana na riba hizo.

Makamu Mwenyekiti wa kamati hiyo, Japhet Hasunga alisema daraja hilo ni muhimu kwa uchumi wa nchi na ujenzi kwa sasa umefikia asilimia 63.



Mkuu wa Wilaya ya Muheza mkoani Tanga, Halima Bulembo (katikati), akiongoza matembezi ya maadhimisho ya Wiki ya Sheria yaliyofanyika mwishoni mwa wiki. Kulia ni Hakimu Mfawidhi wa Mahakama ya Wilaya ya Muheza, Lusajo Mutua. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Polisi yaua wawili wakidaiwa majambazi

**Na Daniel Limbe**

WATU wawili wanaodhaniwa majambazi, wameuawa kwa kupigwa risasi na polisi wilayani Ngara mkoani Kagera huku jeshi hilo likidai kukamata silaha ya kivita aina ya AK 47, risasi 25 na mabomu mawili ya kutupa kwa mkono.

Waliouawa ni wanaume ambao majina yao hayajafahamika na wanakadiriwa kuwa na umri wa kati ya miaka 25 na 30.

Miili ya washukiwa hao wa ujambazi imehifadhiwa kwenye chumba cha kuhifadhi maiti Hospitali ya Nyamiaga kwa ajili ya utambuzi na uchunguzi zaidi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kagera, William Mwampaghale, aliviambia vyombo vya habari jana kuwa tukio hilo lilitokea kwenye Kijiji cha Kumunazi, barabara ya kuelekea Rulenge wilayani Ngara na kwamba jeshi hilo lilipokea taarifa kutoka kwa raia wema kuhusu maandalizi ya uhalifu uliotarajiwa kufanywa na watuhumiwa hao.

Alidai kuwa watuhumiwa hao walipanga kufanya uhalifu wa kutumia silaha kwenye Kijiji cha Kumunazi ili kujipatia mali kwa njia isiyo halali.

"Baada ya taarifa hizo, tuliweka mitego kwenye barabara zote zinazoingia Kumunazi na ilipofika majira ya saa 3:35 usiku, ilipita pikipiki iliyokuwa imebeba watu watatu.

"Baada ya askari wetu kuwasimamisha walikaidi, wakalazimika kupiga risasi hewani ili kuwafanya wajisalimishe lakini waliendelea kupuuza.

"Ndipo askari wakalazimika kuishambulia pikipiki hiyo kwenye matairi ili iishiwe upepo kwa lengo la kuwakamata watuhumiwa hao.

"Kwa bahati mbaya baadhi ya risasi ziliwapata wawili waliokuwa wamebebwa, mmoja alipigwa kwenye paja la kushoto na mwingine kwenye kiuno huku dereva wa pikipiki hiyo akifanikiwa kutokomea porini," alidai Kamanda Mwampaghale.

Alidai kuwa wakati askari wakifanya upekuzi kwenye makoti waliyokuwa wamevaa watu hao, walifanikiwa kukamata silaha moja aina ya AK 47, risasi 25 na mabomu mawili ya kutupa kwa mkono na kwamba jitihada za kutaka kunusuru maisha yao ziligonga mwamba kwa kuwa walifariki dunia wakati wakiwahishwa hospitalini.

Kamanda Mwampaghale alitumia fursa hiyo kuwaonya watu wote wenye nia ya kufanya uhalifu kwenye Mkoa wa Kagera, akisisitiza kuwa doria za magari, pikipiki na miguu zimeimarishwa kwa kushirikiana na polisi wa mikoa jirani ya Geita na Kigoma.

Aniceth Lweyongeza, mkazi wa Ngara mjini, alilipongeza Jeshi la Polisi kwa kudhibiti kwa kiasi kikubwa matukio ya uhalifu wilayani humo, akisema inawafanya waishi kwa amani na kuongeza mwitikio wa uzalishaji mali ili kuinua uchumi wao.

Kagera inatajwa kuwa miongoni mwa mikoa mitano inayoongoza kwa vifo vitokanavyo na uhalifu wa kutumia silaha nchini, huku baadhi ya wahalifu wakidaiwa kutoka nchi jirani kisha kurejea kwao wanapomaliza kutekeleza uhalifu huo.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Utaratibu viongozi kusikiliza kero za wananchi unasaidia kuibua madudu

**KUNA** baadhi ya viongozi ambao wamejiwekea utaratibu wa kukutana na wananchi ili kusikiliza kero zao na kuzitafutia ufumbuzi.

Katika utaratibu huo viongozi wengine huwakaribisha wananchi ofisini kwake na mmoja mmoja huingia na kueleza kero au mapendekezo yatakayowarahishia kuongoza vizuri.

Baadhi yao huamua kufanya ziara kwa kuwatembelea wananchi walipo na kufanya mikutano ya hadhara na hapo hupewa nafasi ya kuuliza maswali au kutaja kero zinazowakabili.

Ziara hizo za viongozi huibua madudu mengi ambayo yalikuwa yamejificha kwa wale wanaoyoyafanya kujiamulia vyovyote wakijua hakuna anayewafuatilia.

Moja ya madudu yaliyoibuliwa katika ziara ya Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, alipotembelea Wilaya ya Manyoni na kuwataka wananchi waeleze kero zao na ndipo aliposimama mwananchi mmoja na kulalamika kuwa baadhi ya madaktari wanakwenda kazini wakiwa wamelewa hali inayowatia hofu kwa usalama wa maisha yao.

Mwananchi huyo alilalamika kuwa alimpeleka mwanawe hospitali na kumkuta daktari akiwa amelewa chakali na kushindwa kuwahudumia. Hali hiyo ya baadhi ya madaktari kufika kazini wakiwa wamekunywa pombe imedaiwa kujitokeza mara kwa mara katika hospitali yao na wananchi kuingiwa hofu ya usalama wa maisha yao.

Kwa kweli hiyo inatia hofu kwa sababu daktari anategemewa katika kumsaidia mgonjwa kujua tatizo lake na kumwandikia dawa ili aweze kupata tiba.

Kama daktari huyo anayetegemewa anafika kazini akiwa hajiwezi kwa kulewa na wagonjwa wakisubiri huduma yake hilo ni tatizo kubwa na halina budi kuchukuliwa hatua za haraka ili wananchi wasaidiwe kuondokana na kero hiyo.

Tabia ya baadhi ya watumishi kuingia kazini wakiwa wamekunywa pombe inapunguza ufanisi wa kazi na vilevile inahatarisha maisha, ustawi wa taasisi au kampuni anayofanyia kazi.

Miongoni mwa watu hao wanaaminiwa na viongozi wao kwa kupewa nafasi za juu, lakini wanashindwa kuonesha ufanisi na kuwaangusha wale waliowapendekeza kushika nafasi hizo.

Mara nyingi watu wa aina hiyo wanapokwenda kutafuta kazi wanakwenda kwa unyenyekevu, lakini wanapozipata wanasahau shida walizopitia na kuanza kuchezea nafasi walizozipata kwa kuingia kazini wakiwa wamechelewa huku wakiwa wamekunywa pombe.

Wengine hudiriki kuondoka kazini huku wakiwa na majukumu mezani mwao ya kufanya na kuchelewesha mipango mingine na kwenda kwenye shughuli nyingine zisizo za kiofisi.


Watu hao huwa wa kwanza kulalamika inapotokea kampuni au taasisi kutikisika kiuchumi na kuamua kupunguza wafanyakazi, akiwa kwenye orodha ya wanaotakiwa kuondoka.

Anasahau kuwa alipokuwa kazini alikuwa akifanya mambo ya ovyo na kutothamini kampuni yake inayomlipa mshahara kila mwezi ambao pengine alikuwa akiwazidi hata wenzake wanaofanyakazi kwa ufanisi na nidhamu.

Ndiyo maana kwa wale waliobahatika kutembelea nchi za wenzetu walioendelea, watu wanalipwa kutokana na kazi wanazofanya. Wengine hudiriki kufanya kazi zaidi ya moja ili aweze kupata kipato zaidi cha kumsaidia kuendesha maisha yake vizuri.

Wewe unayefanyakazi kwa kulipwa mshahara kila mwezi ambao haulingani na kazi unazozifanya ni sawa na kumwibia mwajiri wako kwa kuchukua malipo ambayo hukuyafanyia kazi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Sabato Kasika

## Muungwana Lazima Nilonge

# Msako watoro uibue chanzo

**MOJA** ya mambo yanayosababisha kuwapo kwa maendeleo duni ya wanafunzi darasani, ni utoro ambao unachangiwa na sababu mbalimbali kama majukumu mengine wakati wa masomo.

Sasa ni karibu kila mkoa umetangaza msako wa wanafunzi watoro wanaotakiwa kuanza kidato cha kwanza mwaka huu, hali inayoonyesha kuwa tatizo hilo linazidi kuwa kubwa.

Mfano, wiki iliyopita, madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Songwe waliazimia kufanya msako wa wiki moja wa nyumba kwa nyumba, ili kuwarejesha wanafunzi watoro zaidi ya 1,000 madarasani.

Wakati hao wakiazimia kufanya msakao huo, Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Albert Chalamila naye amewaagiza viongozi na watendaji wote kuanzia ngazi ya mtaa kuanzisha msako kama huo.

Kwa mujibu wa Chalamila, wanafunzi 59,324 walichaguliwa kuingia kidato cha kwanza mwaka huu, lakini walioripiti shuleni ni 35, 594, na kwamba 23,730 wapo mitaani.

Licha ya kuwapo jitihada mbalimbali zinazofanywa ili kukomesha utoro shuleni, ikiwamo msako dhidi ya wanafunzi watoro, inaonekana utoro bado ni miongoni mwa vikwazo vinavyozikabili shule za umma.

Kwa hali hiyo, ni vyema wakati msako wa wanafunzi wa kidato cha kwanza ambao hawajaripoti shuleni ukiendelea, ninadhamini kuna haja pia kutafuta uliko mzizi wa utoro huo na kupatia ufumbuzi wa kudumu.

Ninashauri hivyo, kwa sababu ni karibu kila mkoa umekuwa na matukio ya utoro ambayo yamewafanya viongozi wa mikoa husika kutangaza msako dhidi ya watoto watoro na hata kwa wazazi na walezi wao.

Serikali inatoa elimu bure, wazazi na walezi wanawajibika kuwatafutia watoto wao sare, madaftari na vitu vingine muhimu vya shule, lakini ajabu ni kwamba, pamoja na kuwapo kwa unafuu huo, utoro umeshika kasi.

Ninadhani badala ya kuendelea kutumia nguvu kuwarejesha shuleni, zitumike mbinu ambazo zinaweza kubaini chanzo cha utoro, kisha mbinu zitumiwe kuwarejesha wanafunzi wapende shule.

Lakini kuweka malengo ya kutokomeza utoro na kuweka mbinu ambazo zinawashawishi na kuwavutia wanafunzi kupenda kuhudhuria masomo shuleni, huku wenye tabia ya utoro wakipewa uongozi shuleni.

Kwa ujumla, vivutio vingi kama chakula cha mchana na vipindi vya michezo na hata kuwasaidia wanafunzi wanaofanya utoro kwa sababu ya hali ngumu ya maisha, vinaweza kuwarejesha shuleni.

Baadhi ya wanafunzi watoro wanaweza kuwa ni yatima wanaoishi katika mazingira magumu, wengine ni tabia zao au kwa sababu wanazozijua wenyewe, lakini suala la msingi ni kutafuta mzizi wa utoro ni la muhimu.

Si vibaya vikaanzisshwa vikosi maalum vya kuwatembelea wanafunzi watoro nyumbani, ili kujua kinachosababisha wawe watoro na kama sababu zitakuwa ndani ya uwezo wa vikosi hivyo, basi vizitatue.

Inasikitisha kuona kila mwaka wanafunzi wanaochaguliwa kuingia kidato cha kwanza hawaendi shuleni kwa wakati au wanaingia mitini moja kwa moja na kusababisha kuwapo kwa msako dhidi yao.

Lakini katika kundi hilo la hao wanaoitwa watoro, ninaamini wapo wapo wale ambao wazazi wao wanawahamisha na kuwapeleka katika shule binafsi, bila kutoa taarifa, ingawa idadi yao haiwezi kuwa kubwa.

Pamoja na hayo, ni vyema kuwapo kwa kampeni ya kuhamasisha jamii kuelewa umuhimu wa elimu, kuwaelekeza wazazi na walezi ambao watoto wao ni watoro kutambua manufaa ya elimu.

Katika vita dhidi ya utoro, ni muhumu jamii kutambua umuhimu wa elimu na kungana ili kutofautisha muda wa masomo na muda wa kazi na kuwapunguzia majukumu ya nyumbani, wasiwe watoro.

Inawezekana idadi ya wanafunzi watoro wanaosakwa, wengi wao ni wakike, hivyo kutambua umuhimu wa elimu kunaweza kusaidia kuondoa mtazamo hasi kuhusu kumsomesha binti ni kupoteza pesa.

# Ruvuma, Morogoro sasa kuunganishwa kwa lami

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

SERIKALI inatarajia kuanza mradi wa kuiunganisha mikoa ya Ruvuma na Morogoro kwa barabara ya lami.

Ruvuma ni miongoni mwa mikoa nchini ambayo tayari wilaya zake zote zimeunganishwa kwa lami na makao makuu ya mkoa.

Meneja wa Wakala wa Barabara (TANROADS) Mkoa wa Ruvuma, Ephatar Mlavi, alisema jana mjini hapo kuwa serikali inatarajia kutekeleza mradi wa ujenzi wa barabara ya Lumecha – Londo wilayani Namtumbo mkoani Ruvuma hadi Kilosa-Kidatu mkoani Morogoro kwa kiwango cha lami.

Mlavi aliutaja mradi huo kuwa utahusisha ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami yenye urefu wa kilometa 512 ambao ukikamilika utaunganisha Mkoa wa Ruvuma na Morogoro kwa kiwango cha lami.

"Mradi huu upo katika hatua ya kupitia zabuni za makandarasi ambazo zilifunguliwa tarehe 26, Agosti 2022. Mradi huu utatekelezwa kwa kutumia mfumo wa usanifu, ununuzi, ujenzi na ufadhili)," alisema Mlavi.

Meneja huyo alisema utekelezaji wa mradi huo unatarajiwa kuanza muda wowote baada ya hatua stahiki za ununuzi kukamilika.

Akizungumzia ujenzi wa Barabara ya Songea – Makambako kwa kiwango cha lami, Mlavi alisema serikali inatarajia kutekeleza mradi wa ujenzi wa barabara ya lami sehemu ya Songea – Lutukira ikijumuisha na sehemu ya Mtwara Korido yenye urefu wa kilometa 111.

Mlavi alisema kuwa katika utekelezaji wa mradi huo, serikali tayari imeshaingia makubaliano na mfadhili ambaye ni Benki ya Dunia na mradi huo sasa upo katika hatua za awali za ununuzi.

Alibainisha kuwa mradi huo utahusisha ujenzi wa kilometa 111 za lami ambazo zitajumuisha kilometa 14 za Songea bypass kwenye Manispaa ya Songea na ujenzi wa barabara ya Songea hadi Lutukira Halmashauri ya Madaba yenye urefu wa kilometa 97, hivyo kuunganisha Wilaya ya Songea mkoani Ruvuma na Wilaya ya Njombe mkoani Njombe.

Alisema Mkoa wa Ruvuma kupitia Wilaya ya Nyasa tayari umeunganishwa na Mkoa wa Njombe kupitia Wilaya ya Ludewa kwa kutumia daraja la Mto Ruhuhu unaomwaga maji yake Ziwa Nyasa.

Alisema mradi wa daraja la Ruhuhu ulianza kutekelezwa Juni 2016 na kukamilika Oktoba 2021 kwa gharama ya zaidi ya Sh. bilioni 8.9 ambao umeunganisha wilaya za Nyasa na Ludewa.

Katika mwaka wa fedha 2022/23, TANROADS Mkoa wa Ruvuma iliomba bajeti ya zaidi ya Sh. bilioni 41 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Zaidi ya Sh. bilioni 28 ndizo zimeidhinishwa kwenye bajeti ya mwaka huu wa fedha.




Moja ya magari ya Kampuni ya MIGHTY Logistic likishusha shehena ya makaa ya mawe kwenye Bandari ya Mtwara tani 55,000 kutoka Kampuni ya Jitegemee Holding ya mkoani Ruvuma yakisafirishwa nchi za Ubelgiji, Ufaransa na Hispania. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# DC aagiza msako nyumba kwa nyumba wasioripoti shuleni

**Na Steven William,** MUHEZA

MKUU wa Wilaya ya Muheza mkoani Tanga ameagiza kuwasaka wanafunzi ambao hawajaripoti shuleni licha ya kuchaguliwa kujiunga na kidato cha mwaka huu ili hatua zichukuliwe dhidi ya wazazi wao.

Halima Bulembo alitoa agizo hilo jana alipohutubia kwenye ufunguzi wa mkutano wa wadau wa elimu Wilaya ya Muheza uliofanyika mjini hapo.

Alisema wilaya hiyo hadi sasa imeandikisha asilimia 76 ya wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka huu.

Halima alibainisha kuwa wanafunzi wapatao 1,064 hawajaripoti shuleni. Kati yao, wavulana ni 569, akiagiza wanafunzi hao kusakwa nyumba kwa nyumba.

Alisema wazazi, walimu na walezi wawe walinzi wa watoto wao kwa kuwa hivi sasa wananajisiwa na kulawitiwa, hivyo wanapoona jambo kama hilo, watoe taarifa polisi ili watu wenye tabia hiyo wakamatwe.

Mkuu wa Wilaya pia aliagiza wazazi wote kuchangia chakula kwa ajili ya watoto wao wawapo shuleni, huku akiwataka madiwani na viongozi wengine kuhamasisha kuchangia chakula shuleni.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza, Emigidius Kasunzu, alisema wilaya hiyo imepokea Sh. milioni 62 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa na mpaka sasa Sh. milioni 25 zimetumika.

Alisema Halmashauri ya Wilaya ya Muheza imepokea Sh. milioni 900 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu katika shule za msingi na sekondari.

Ofisa Elimu wa Shule za Msingi Wilaya ya Muheza, Pili Maxmiliani, alibainisha kuwa wanafunzi waliofaulu kujiunga kidato cha kwanza ni 6,500 na kwamba 1,064 hawajaripoti shuleni.

Alisema kuwa katika suala la elimu Wilaya ya Muheza wamefanya vizuri katika ufaulu kila mwaka lakini kuna changamoto mbalimbali ukiwamo upungufu wa walimu na madawati na uchakavu wa miundombinu ya shule.

Alisema Wilaya ya Muheza inakabiliwa na tatizo la utoro kwa wanafunzi linalosababisha kufeli kwenye mitihani ya taifa.

Ofisa Elimu wa Sekondari Wilaya ya Muheza, Fredence Serapion, alisema lengo la mkutano wa wadau wa elimu ni kujadili namna ya kuinua kiwango cha elimu wilayani hapa.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Muheza, Erasto Mhina na Katibu Tawala Wilaya, Desderia Haule, kwa nyakati tofauti waliwapongeza wadau wa elimu waliofika kwenye kikao hicho kujadili masuala ya elimu.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# Tz yasifiwa kuongeza wanawake viongozi kwenye vyombo vya habari

**Na Elizabeth Zaya**

UTAFITI uliofanywa na Taasisi ya Women in News (WIN) kuhusu ombwe la viongozi wanawake kwenye vyombo vya habari, kumebaini kuwa kwa nchi za Afrika, Tanzania inafanya vizuri kwa kuwa na idadi kubwa ya viongozi wanawake.

Naibu Mkurugeni Mkuu wa Women in News kwa upande wa Afrika, Jane Godia, amesema katika utafiti walioufanya kwa nchi 17 duniani mwaka 2022 wamebaini kuna ombwe kubwa la viongozi wanawake katika vyombo vya habari na kwamba upo umuhimu wa kuwa na usawa wa kijinsia katika uongozi.

Godia aliyasema hayo juzi kwenye mkutano wa uzinduzi wa Women in News Alumni Tanzania, uliofanyika jijini Dar es Salaam.

Alisema katika utafiti huo walibaini kwa nchi za Afrika, Tanzania ndiyo inafanya vizuri kwa kuwa na asilimia 10 ya wanawake wanaongoza kwenye vyombo vya habari na katika nafasi ya uhariri ni asilimia 56. "Tukahakikisha kwamba tunaweka programu maalum ya kuwajengea uwezo wanawake katika eneo hilo ili kuweka usawa wa kijinsia katika uongozi kwenye kwenye vyombo vya habari," alisema Godia.

Akifungua mkutano huo, Msemaji wa Serikali, Gerson Msigwa, alisema ni vyema vyombo vya habari vikajenga utamaduni wa kuwa na mafunzo ya ndani ya kujengea uwezo, kuwa na sera za jinsia pamoja na kuhakikisha wanawake wenye uwezo wanaaminiwa na kupewa nafasi za kuongoza vyumba vya habari.

"Natambua baadhi ya vyombo vya habari havina sera ya ambayo pamoja na mambo mengine ingetoa mwongozo wa namna nzuri ya kuhakikisha wanawake na wanaume wanafanya kazi katika mazingira rafiki na wakapata haki sawa ikiwa ni pamoja na wale wenye uwezo wa kuongoza kupata nafasi za juu," alisema Msigwa.

"Natambua wapo baadhi ya wakurugenzi watendaji kwenye vyombo hivi, baadhi yenu humu ni wahariri watendaji, wahariri wa habari na viongozi wa taasisi za habari, lakini idadi yenu bado ni ndogo ikilinganishwa na wanawake waliopo kwenye tasnia wanaoweza kutekeleza wajibu wao.

"Tunaamini kuwa na waandishi wa habari wengi wanawake wanaotekeleza majukumu yao vyema, kutabadilisha mtazamo hasi wa jamii kuwahusu, kuondoa mazoea ya kwamba chumba cha habari ni dunia ya wanaume lakini pia vyanzo vya habari ambavyo ni wanawake vitaongezeka."

Alisema habari iliyoandaliwa kwa kushirikisha jinsi zote inayozungumzia yanayohusu wanaume na wanawake ina uwezekano mkubwa wa kuleta matokeo chanya kutokana na kubeba mtazamo wa jamii nzima.

"Kwa ngazi ya taifa, tayari tunafanya vizuri, tuna Rais wa kwanza mwanamke, Rais Samia Suluhu Hassan, na kwenye Mhimili wa Bunge tuna Spika mwanamke, Dk. Tulia Akson, lakini kwenye Baraza la Mawaziri, tuna wanawake ambao wote wanafanya vizuri kwenye nafasi zao," alisema Msigwa.

Alisema Tanzania imebeba agenda ya kumwinua mwanamke katika ngazi mbalimbali na vyombo vya habari navyo vinapaswa kuunga mkono hilo kwa kuwaamini wanawake wenye uwezo kuwapa nafasi.

"Nina amini kama tumefanikiwa kuwa na kiongozi imara, shupavu na mchapakazi Rais Samia, basi vyombo vya habari vinapaswa kuiga mfano huu kwa kuwapa nafasi wanawake wenye uwezo kuongoza ili kuleta mabadiliko chanya kwenye jamii.

"Serikali inawahakikishia waandishi wa habari mazingira ya uhuru katika utekelezaji wa majukumu. Natoa wito kwa wamiliki wa vyombo vya habari nchini kuunga mkono ajenda ya jinsia na kuitekeleza kwa vitendo ili tunapofika kwenye vyombo vya habari tuone idadi ya wanawake wenye nafasi za uongozi ambao watawavuta wengine na kuonyesha kuwa hata kwenye uandishi wa habari wanawake wanaweza kufanya vitu vizuri.

"Serikali inawahakikishia ushirikiano mkubwa kwenye utekelezaji wa majukumu yenu na milango ya Idara ya Habari (MAELEZO) iko wazi muda wote kwa ajili ya kuhakikisha tasnia ya habari inazidi kustawi nchini."



Ofisa Mawasiliano wa Taasisi ya Legal Services Facility, Wilson Mtapa (kushoto), akimpa huduma mteja, Shaban Ndege, aliyetembelea banda hilo wakati wa maadhimisho ya Wiki ya Sheria yanayoendelea katika Viwanja vya Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu Dar es Salaam jana. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# RC ataka mahakama uadilifu katika usuluhishi wananchi

**Na Halima Ikunji,** TABORA

MKUU wa Mkoa wa Tabora, Dk. Batrida Buriani, ameagiza watumishi wa Mahakama Kuu kufanya kazi ya usuluhishi na kupatanisha wananchi kwa uadilifu.

Alitoa kauli hiyo jana mkoani hapo katika siku ya wiki ya sheria nchini na kuwataka watumishi hao watende haki wanapo suluhisha mambo makubwa kwa kutumia hekima.

Alitaka watumishi wa mahakama hiyo kupitia uzinduzi wa wiki ya sheria nchini kutimiza majukumu yao kama ilivyoelekezwa ili kazi zao ziwe na tija kwa wananchi wao.

Dk. Buriani alipongeza Mahakama ya Wilaya ya Tabora kwa kutoa hukumu kwa mkazi wa Kidatu 'B' Kata ya Mtendeni mkoani Tabora, Husseni Nasibu Mashibu (32) kwenda jela maisha kwa kosa la kumlawiti mtu mzima hadharani.

Alisema kesi hiyo ilitolewa hukumu na Hakimu Mkazi Mwandamizi wa Mahakama ya Wilaya ya Tabora, Msigwa Mzige, Januari 16, mwaka huu.

"Mahakama mmefanya vizuri kwa kutoa hukumu hiyo ambayo imeendana na kosa alilotenda mtuhumiwa na kifungo hicho kimefanana na tendo lake," alisema.

Alisema migogoro mingi inasababishwa na wananchi wanaotoa taarifa za uongo kutoka familia moja na kwenda nyingine.

**Alisema kesi hiyo ilitolewa hukumu na Hakimu Mkazi Mwandamizi wa Mahakama ya Wilaya ya Tabora, Msigwa Mzige, Januari 16, mwaka huu.**

# Shirika lasaidia vishikwambi maofisa elimu

**Na Thobias Mwanakatwe,** IKUNGI

SHIRIKA la Farm Africa kwa ushirikiano na Shirika la Umoja wa Mataifa la UN-Women chini ya ufadhili wa Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Korea (KOICA), limetoa vishikwambi na simu janja kwa maofisa ugani na wakulima wilayani Ikungi, mkoani Singida.

Waliopewa vishikwambi hivyo ni kutoka kata za Sepuka, Dun'gunyi na Irisya na wakulima ni Asha Budo na Zainabu Hussein kutoka kijiji cha Sepuka.

Wengine ni Zainabu Mbua na Frida Kikohozi kutoka kijiji cha Dung'unyi, Elizabert Kitua wa kijiji cha Munyu na Mwanaisha Bakari wa kijiji cha Irisya.

Meneja Mwandamizi wa Shirika la Farm Africa, Tumaini Elibariki, alisema vifaa hivyo vimetolewa ili visaidie huduma za ugani na utafutaji wa masoko ya ndani na nje kwa mazao wanayozalisha.

"Vifaa hivyo vitawasaidia kueleza masuala ya kilimo biashara hususani elimu ya ugani, taarifa za masoko, utunzaji wa kumbukumbu na mawasiliano na wanunuzi wa mazao yanayozalishwa na wakulima," alisema.

Katika hafla ya kukabidhi vishikwambi hivyo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, Justice Kijazi, alilishukuru Shirika la Farm Africa na washirika wake kwa jitihada inazofanya kuinua kilimo kwa wananchi katika wilaya hiyo.

Kijazi alisema halmashauri yake itaendelea kushirikiana na wadau wanaosaidia wakulima ili kuinua sekta ya kilimo ambayo ndio inatoa ajira kubwa kwa wananchi.

Katibu Tawala Wilaya ya Ikungi, Winfrida Funto, ambaye alikuwa mgeni rasmi katika hafla hiyo, aliwataka wakulima na maofisa ugani waliopewa vifaa hivyo kuvitunza na kuvitumia katika malengo yaliyokusudiwa ili kuleta mageuzi katika sekta ya kilimo.

Funto alipongeza Farm Africa kwa kipaumbele kuwajali wanawake na kuwasaidia katika masuala ya kilimo utaratibu uliowavutia wanawake wengi kupenda kilimo na kujikwamua kiuchumi.





## Kimbunga chaezua paa za nyumba, kaya sita zalala nje

**Na Cynthia Mwilolezi,** BABATI

KAYA zaidi ya sita za Tarafa ya Bashnet, Wilaya Babati, mkoani Manyara, hazina mahali pa kuishi baada ya kimbunga kilichoambatana na upepo mkali, kuezua paa za nyumba zao pamoja na zile zinazomilikiwa na taasisi za serikali.

Mpaka sasa hakuna majeruhi wala vifo vilivyoripotiwa katika vijiji vinavyounda tarafa hiyo, zaidi ya hasara ya mali.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Babati, Anna Mbogo ajali hiyo ilitokea juzi majira ya jioni.

Mbogo alisema kati ya nyumba sita zilizoezuliwa paa nyumba mbili ni za Hospitali ya Buma zilizoko vitongoji vya Kwankwar na Bashnet.

Alisema upepo huo mkali ulioambatana na kimbunga, uliezua mabati ya nyumba hizo na kuangusha miti, baada ya mvua kunyesha kwenye maeneo hayo ya Tarafa ya Bashnet.

"Mimi na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Babati (John Noya), tulitembelea eneo hilo na kutoa pole kwenye nyumba hizo sita," alisema.

Alisema Halmashauri ya Wilaya hiyo, imetoa Sh.milioni mbili kwa ajili ya kuwapa wananchi waliokumbwa na janga hilo la nyumba zao kuezuliwa paa.

Aidha, akizungumzia ajali hiyo, Mbunge wa Babati Vijijini, Daniel Sillo, alitoa pole kwa wananchi hao waliokumbwa na majanga hayo kwa kuwakabidhi mabati 85.

Mmoja kati ya wakazi wa Kitongoji cha Kwankwari, Richard Hans, alisema upepo huo umesababisha hasara ya mazao yake ya mahindi madogo yaliyokuwa yaanza kumea.

# Serikali yang'atwa sikio biashara ya maji, mafuta, chumvi kanisani

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

NABII Mkuu wa Kanisa la Ngurumo ya Upako, Dk. Geordavie Kasambale, ameipa somo Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kufanya uchunguzi wa 'kimya kimya' ya makanisa yanayouza maji, mafuta na chumvi, kwa madai kuwa kinachofanyika ni biashara ya kuuza bidhaa na utapeli wa imani.

Dk. GeorDavie, alisema asilimia kubwa ya makanisa hayo yanapotosha jamii pamoja na kutumia mgongo huo, kukwepa kodi ya serikali.

Alitoa ushauri huo juzi jijini Arusha, wakati akiongea na waumini wa kanisa hilo. Alisema baadhi ya makanisa hayo, viongozi wake wamekuwa wakitumia visaidizi hivyo kuwadanganya waumini na mbaya zaidi wamekuwa wakitumia mgongo wa kanisa kufanya biashara.

"Ni vyema kanisa likabaki ni mahali pa kutoa na kufundisha neno la Mungu na sio sehemu ya kufanya biashara, kama baadhi ya viongozi wa dini wanavyofanya biashara za kuwauzia waumini visaidizi kama mafuta, chumvi, juice, sabuni na vinginevyo.

"Nipende kuwaambia tu baadhi ya viongozi wa dini, kama nguvu ya Mungu ipo ndani yako, itabaki nguvu za Mungu na kanisa litaendelea. Hata ukifuatilia kwenye vitabu vyetu vya dini, hakuna sehemu ambayo inasema Yesu aliuza mafuta, maji, wala chumvi katika kipindi chake.

Zaidi aliongeza: "Wala hakuna Mahali Yesu aliwakusanya watu wakafa kisa kugombania mafuta, niseme tu wanaofanya hivyo ni matapeli tu hivyo ni vyema watu wakaamka wakasimama kwenye msingi wa zamani ambao ni neno la Mungu," alisema Nabii Mkuu Dk. Geordavie.

Kutokana na maono yake, amesisitiza kuwa wakati umefika kwa Watanzania na waumini, kuachana na visaidizi na waridhike na nguvu za Mungu wanayohubiriwa na wachungaji wao.

Alisema kuwa iwapo serikali itaendelea kuwaachia viongozi hao kufanya vitu hivyo, iko siku maafa makubwa yanaweza kutokea kwa kuwa hata maafa yaliyotokea katika baadhi ya nchi, yaliyotokana NA viongozi wa dini kuwachanganya waumini wao.



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Manyara Kamishna Msaidizi wa Polisi, George Katabazi, akiwaonesha waandishi wa habari meno ya tembo yenye thamani ya zaidi ya shilingi milioni nane ambayo waliyakamata katika kijiji cha Matufa wilayani Babati mwishoni mwa wiki. **PICHA: JALIWASON JASSON**

# Wadau EAC kushirikiana mapambano magonjwa ya mlipuko

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

WADAU wa maendeleo kutoka mashirika ya kimataifa, benki za maendeleo na nchi sita wanachama wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki (EAC), wameweka alama ya kwanza ya ushirikiano wa pamoja wa kushughulika na magonjwa ya milipuko katika ukanda huo.

Hatua hiyo imekuja baada ya kukutana na kujadili utekelezaji wa Mpango wa Afya ya Pamoja (GP PPOH), unaofadhiliwa na serikali ya Ujerumani.

Akizungumza jana jijini Arusha, wakati wa mkutano wa kwanza wa jukwaa la washirika wa mpango wa afya ya pamoja (OH), Ofisa Mwandamizi wa Mifugo wa Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Dk. David Balikowa, alisema magonjwa yanayopewa kipaumbele cha kukabiliana nayo katika ukanda huo ni ebola, virusi vya corona na kipindupindu.

"Tumekutana hapa wadau 100, kujadili na kuainisha mikakati ya kuzuia magonjwa ya milipuko. Kwa miongo miwili iliyopita Jumuiya ya Afrika Mashariki, imekumbwa na magonjwa ya kuvuka mpaka na kushuhudia athari zake katika sekta nyingi zikiwamo za uchumi na biashara.

"Huu unakuwa mkutano wa kwanza wa mwaka wa wadau wa sekta ya afya kutoka nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, ambao unatokana na mapendekezo ya timu ya wataalamu kutoka jumuiya hii," alisema Dk. Balikowa.

Mkakati wa OH wa EAC, ulikubaliwa Novemba mwaka 2021 kwamba GP PPOH ingesaidia maandalizi na utekelezaji wa jukwaa la washirika, mara mbili kwa kila mwaka ili kutimiza madhumuni ya kuongeza ushirikishwaji wa wadau wa mpango huo.

"Kutokana na mapendekezo hayo, EAC imeandaa mkutano huu kwa lengo la kupanga utekelezaji wa pamoja wa mikakati kuhusu kushughulika na magonjwa ya kuambukiza na yasiyo ya kuambukiza miongoni mwa nchi wanachama," alisema.

Katika mkutano huo, Mtaalamu wa Afya ya Mifugo kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu (Tanzania), Dk. Baltazar Leba, alisema jukwaa hilo la washirika, limeketi ili kukuza uelewa juu ya utekelezaji wa mpango wa afya ya pamoja, kwa washikadau walioko au wanaofanya kazi katika eneo hilo.

Aidha, Dk. Leba, alisema nia ya jukwaa hilo kukutana ni kutaka kukuza uwezekano wa kuimarishwa kwa uratibu na ushirikiano wa wadau katika ukanda huo na kutambua fursa madhubuti katika mpango huo.

Mkurugenzi wa sekta za jamii kutoka Jumuiya ya Afrika Mashariki, Dk. Irene Isaka, akichangia mjadala kuhusu utekelezaji wa mpango huo, alisema jukwaa hilo limeweka alama ya kuwa mwanzo wa ushirikiano wa pamoja wa kushughulika na magonjwa ya milipuko.

"Ushiriki wenu mzuri katika jukwaa hili la kwanza la wadau wa afya ya pamoja kutoka Jumuiya ya Afrika Mashariki ni kuonyesha dhamira ya dhati ya kushirikiana katika kuzuia na kukabiliana na magongwa ya milipuko katika ukanda wetu. Na huu ni msingi bora wa ushirikiano utakaoendelea kila mwaka katika siku zijazo," alisema Dk. Isaka.

Jukwaa hilo la pamoja liliwashirikisha wadau mbalimbali duniani, likiwamo Shirika la Kimataifa linalojihusisha na Afya ya Wanyama (WOAH), Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa (UNEP), Shirika la Kudhibiti Magonjwa ya Maambukizi Barani Afrika (Afrika CDC) na Benki ya Dunia (WB).

Wadau wengine ni Benki ya Wananchi wa Ujerumani (KFW), Serikali ya Marekani, kupitia Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID), Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) na Shirika la Uhamiaji la Umoja wa Mataifa (UN Migration).



# Jeshi la Polisi laanza operesheni ya kuwasaka wezi wa vifaa SGR

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

JESHI la Polisi mkoani Shinyanga limeanza kutekeleza agizo la Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, la kuwasaka watu wanaojihusisha na vitendo vya wizi wa mafuta na vifaa vya ujenzi katika mradi wa Reli ya Kisasa (SGR) kipande cha Tabora- Isaka.

Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Shinyanga, Janeth Magomi, aliyasema hayo jana wakati akitoa taarifa kwa vyombo vya habari kuhusu msako waliofanya ndani ya mwezi mmoja na kukamata vitu mbalimbali vya wizi zikiwamo nyara za serikali.

Dk. Mpango alipokuwa mkoani Shinyanga kuweka jiwe la msingi la ujenzi SGR aliagiza watu wanaohujumu mradi huo wasakwe na wakamatwe.

"Jeshi la Polisi mkoani Shinyanga tunaendelea kutekeleza maagizo ya Makamu wa Rais juu ya watu ambao wanaendelea kuhujumu mradi wa SGR na tunaendelea kuyasimamia na tumekamata watu 10, pikipiki zilizokuwa zikitumia katika wizi na mipira ya kunyonyea mafuta na madumu 42 na mafuta ya petroli lita 225," alisema Magomi.Aliongeza: "Tumepokea pia maelekezo kutoka kwa Mkuu wa Jeshi la Polisi na juzi walifika makamishna wawili, Kamishna wa Polis Jamii na Operesheni na Mafunzo ambao wamekuwa wakitoa msisitizo wale wote wanaohusika kuhujumu ujenzi wa reli wakamatwe na wachukuliwe hatua wakiwamo askari polisi".

Wakati huohuo, Kamanda Magomi alisema jeshi hilo linawashikilia watu wengine watatu kwa wizi wa nyara za serikali zikiwamo mikia ya nyumbu 21, maganda matano ya mayai ya mbuni, ngozi za paka pori, miba 44 ya nungunungu, vipande vitatu vya mkonga wa tembo, mikia mitatu ya ngiri, vipande vitatu vya magamba ya kobe. Alitaja nyara zingine ni kucha tano za paka pori, kipande kimoja cha jino la tembo, ngozi ya fungo na pembe ya korogo na kwamba upelelezi unaendelea na ukikamilika watuhumiwa watafikishwa mahakamani.

Vingine ni mita moja ya Shirika la Umeme Nchini (TANESCO), television nne, subufa moja, seti moja ya muziki, pombe haramu ya gongo lita 10, nyaya za mawasiliano za TTCL.

Aidha, alisema katika kesi mbalimbali watuhumiwa wamefungwa jela ikiwamo kesi ya ubakaji, ukatili wa mtoto, upatikanaji wa bangi, huku akiwasihi wananchi kuacha vitendo vya uhalifu pamoja kujichukulia sheria mkononi.



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Janeth Magomi, akionyesha madumu waliyoyakamata yakitumika kuiba mafuta katika mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) mkoani humo jana. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Polisi yaua wawili wanaodhaniwa ni majambazi

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

JESHI la Polisi mkoani Kagera limewaua kwa kuwapiga risasi watu wawili wanaodaiwa kuwa ni majambazi.

Pia limekamata bunduki moja aina ya AK 47 ikiwa na magazine moja yenye risasi 25 pamoja na mabomu mawili ya kutupwa kwa mkono.

Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Kagera, William Mwampaghale, alisema kuwa tukio hilo lilitokea baada ya kupata taarifa Janauri 21, mwaka huu kutoka kwa raia wema kuwa kuna watu wanasafirisha silaha kwa kutumia pikipiki.

Alisema baada ya kupata taarifa hiyo waliweka mtego katika barabara zote zinazotoka na kuingia katika Mji wa Ngara.

Kamanda huyo alisema kuwa ilipofika saa 3:35 usiku katika barabara itokayo eneo la Kumnazi kuelekea Rulenge wilayani humo, walionekana watu watatu wakiwa kwenye pikipiki moja.

Alisema polisi waliokuwa doria waliwasimamisha lakini watu hao hawakutii amri badala yake waligeuza pikipiki na kuanza kukimbia.

Alisema kuwa polisi walifyatua risasi hewani na kuwasihi wasimame lakini watu hao hawakusimama hivyo walilazimika kufyatua risasi kwa dhumuni la kupiga tairi la pikipiki.

Kamanda huyo alisema kwa bahati mbaya risasi hizo ziliwapata abiria wawili waliokuwa wamebebwa kwenye pikipiki hiyo.

"Walipopigwa risasi walidondoka chini na yule mmoja aliyekuwa akiendesha alifanikiwa kukimbia, tulipowafikia na kuanza kuwapekua tukakuta wana bunduki hiyo aina ya AK47, ikiwa na magazine moja yenye risasi 25 na pia tukakuta wana mabomu mawili ya kutupwa kwa mkono," alisema.

Alisema kuwa jitihada za kuwawahisha hospitali zilifanyika, lakini kutokana na majeraha makubwa ya risasi waliyoyapata walipoteza maisha wakati wakiwa njiani.

Alisema miili yao imehifadhiwa katika Hospitali ya Nyamiaga iliyoko wilayani Ngara.

Mwampaghale alisema kuwa kuuawa kwa watu hao na kupatikana kwa silaha hizo kumetokana na operesheni inayoendelea katika Mkoa wa Kagera kwa kushirikiana na vyombo vingine vya dola katika mikoa jirani ya Shinyanga, Kigoma na Geita.

"Watu wote wanaojihusisha na uhalifu Kagera hususani wa kutumia silaha nawatahadharisha waache mara moja maana operesheni ni endelevu kwa hiyo wakiendelea wajue watakamatwa na kufikishwa katika vyombo vya sheria," alisema.

Aidha, aliwataka wananchi kuendelea kutoa ushirikiano kwa jeshi hilo juu ya watu wanaojihusisha na uhalifu ili hatua za haraka zichukuliwe kabla ya kuleta madhara.

## Akutwa amejinyonga huku ameshika shela la mkewe

**Elizabert Seleman,** SENGEREMA

MKAZI wa Kata ya Nyatukala wilayani Sengerema mkoani Mwanza, Masaga Kumbi (38) amedaiwa kujinyonga hadi kufa kwa kutumia kamba, huku akiwa ameshikilia shela alilovaa mke wake siku ya harusi yao.

Akizungumza na waandishi wa habari kuhusu tukio hilo, mmoja wa ndugu wa marehemu, Tabu Mhoja alisema wamesikitishwa na kitendo ambacho amekifanya ndugu yao na kuwashauri vijana wanapopata matatizo kwenye ndoa wanatakiwa kushirikisha watu kwa msaada zaidi.

Alisema ndugu yao alifunga ndoa mwishoni mwa mwaka jana na kipindi chote waliishi kwa furaha na mke wake, lakini wameshangazwa kumuona amejiua tena akiwa ameshikilia vazi la harusi la mkewe.

Baadhi ya watu walioshuhudia tukio hilo, walisema uamuzi aliochukua Masaga haukuwa sahihi na kusema kwamba vijana wanapopatwa na matatizo wanatakiwa kuwashirikisha watu wao wa karibu.


Aidha, alisema kwenye ndoa kuna matatizo, kwamba unapokuwa na shida yoyote hupaswi kunyamaza na kukaa na jambo rohoni.

Akizungumzia tukio hilo, Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Geita, Pelana Bagume alisema Masaga alikutwa eneo hilo akiwa tayari amefariki.

Hivyo aliwataka watu wanaokutwa na shida mbalimbali kuwashirikisha ndugu ama marafiki waliowazidi umri ili wapate ushauri badala ya kuchukua uamuzi wa kujiua.

Pia aliwataka watu kuwa na hofu na Mungu kwa maana yeye ndiye anayetoa uhai na siyo wanadamu kujichukulia jukumu la kujiua.

Jeshi la Polisi wilayani Sengerema walifika na kuubeba mwili wa marehemu kwa ajili ya kuupeleka katika chumba cha kuhifadhia maiti Hospitali ya Wilaya ya Sengerema.




Ukurasa 12

Teknolojia kidigitali inavyopunguza safari za nenda rudi kwenye ofisi



Ukurasa 13

Kushawishi watoto kujifelisha mitihani kunavyoimaliza Pwani

Nipashe
# TESA
Jumanne Januari 24, 2023
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 14

## Iringa yawa 'kuzimu' kwa watoto, taifa la kesho lawekwa hatarini

ELIMU

NA MWANDISHI WETU

# Ujio madawati jinsia vyuoni uambatane na bidii, si kusubiri fadhili, maksi za bure

ZIPO taarifa za kuongezeka vitendo vya unyanysaji kingono hasa kwa wasichana wanafunzi wa vyuo vya kati na vya elimu ya juu, hatua kadhaa zikichukuliwa mojawapo ni kuanzishwa kwa madawati ya jinsia kwa kila chuo ili kukabiliana na tatizo hilo.

Hali hii imekuwa ikivuta masikio ya wengi kwani kuongezeka kwake ni kuzidi kuongezeka kwa vitendo hivyo ni kuongeza hatari ya kundi hili la vijana kupata maambukizi ya magonjwa ya ngono hasa VVU na UKIMWI, homa ya ini na hata saratani ya shingo ya uzazi.



Juhudi za kujifunza kwa bidii na kupata shahada zinahitajika sanjari na madawati ya jinsi vyuo vya kati na vya elimu ya juu. **PICHA: MTANDAO**

### CHANZO

Kama ilivyo kwenye matatizo mengine, kuna sababu nyingi za kuongezeka kwa vitendo vya ngono na unyanyasaji hasa katika taasisi za elimu ya juu kwa maana vyuo vya kati na vyuo vikuu. Mojawapo ya ni tamaa za baadhi ya watu hasa wahadhiri wakitaka kufanya mapenzi na wanafunzi wao.

Hili halina cha umri wa jinsia ya mwalimu ila ni tabia ya kuwa na tamaa, kukosa hofu ya Mungu na maadili mema kwa mtuhumiwa au mhadhiri.

Ambao kimsingi ni wazazi wao kwa maana ya nafasi na umri wao wanatakiwa kuwa walezi au wazazi bora wa mwanafunzi vyuoni. Sababu nyingine kubwa ni wanafunzi kukosa bidii katika kujifunza na kutafuta maarifa hivyo kusubiri fadhila za walimu wao kwa maana wahadhiri kuwapa maksi za bure lakini wengine wakifikiria kuwapa ngono.

Mfano, tabia hii imekuwa zaidi kwa wanafunzi wasichana hasa kwa kudhani kuwa wana maumbile mazuri, sura nzuri, lakini hawajitumi katika kusoma bali wanasubiri kwenda kwa walimu ili kuomba kupewa na kuongezewa maksi za upendeleo ili kuweza kukidhi kiwango cha ufaulu unaotakiwa lakini wakitumia sifa hizo.

Muda mwingine ili kupata maksi nyingi zaidi hata kuwapita wale waliosoma vizuri na kufaulu kwa juhudi zao wenyewe, huchochea uwepo wa matendo ya ngono vyuoni.

### MATOKEO NI NINI?

"Ukitaka cha bure lazima uteseke," Tabia hii ya baadhi ya wanafunzi kupenda kupewa maksi za upendeleo kutoka kwa walimu wao bila kuzifanyia kazi kwa maana ya kusoma kwa bidii, huleta matokeo hasi kwao. Kwa mafano baadhi ya walimu na wahadhiri kuamua kutumia mwanya huo kutimiza nia zao ovu hasa za kufanya ngono na kuwaambukiza maradhi, kupata mimba, wengine kuzitoa lakini kujishushia heshima.

Hii ni kwasababu mwanafunzi anakuwa katika hali ya uhitaji wa msaada, hilo huwa ni takwa mojawapo ili kuongezewa maksi tena za bure bila kutoka jasho, wengi wao baada ya kupata maksi hizo huanza kutamba kwa wenzao kuwa walijifanya kusoma lakini wamewezidi au wamepata maksi sawa. Hilo huongeza kukata tamaa kwa baadhi ya wanafunzi na kuamini kuwa njia ya kufanya vizuri katika masomo ni kuwa na mahusiano ya kimapenzi na wahadhiri.

Wanafunzi wengi hasa wale wa kike wasio na malengo binafsi huanza kuiga na kujiingiza katika tabia hiyo ya kuwafuata fuata na kuwashawishi walimu ili kuwa na uhusiano nao kimapenzi kwa kutegemea kupendelewa kwenye masomo yao.

### MADHARA KIJAMII

Yapo madhara mengi ya tabia hiyo kwa jamii kwa mfano; wanachuo wengi wanakesha kwenye kumbi za starehe wakinywa pombe, kucheza muziki na kujihusisha na vitendo vya ngono. Hii hufanya wanafunzi hao kurudi usiku wa manane au asubuhi kushindwa kufika darasani kwasababu ya uchovu na hali ya ulevi.

Zaidi wanafunzi hawa hawafanyi kazi wanazopewa na walimu kwasababu za uzembe au kutojua nini cha kuandika kwani kipindi mada zinafundishwa hawakuwapo kwenye mihadhara.

Hivyo wasomi hawa wa kike huingia katika mitego ya uhusiano wa kimapenzi na kufanya michezo hiyo na walimu, wahadhiri wao, wanaume wengine mitaani ili kupata pesa zaidi na maksi ambazo hawakustahili ila kwa upendeleo ambao ni hasara kwao na taifa.

Upendeleo ambao una masharti magumu ya kufanya ngono kama malipo ya maksi hizo za bure, athari za muda mrefu ni kupata wasomi wanaopewa mikopo na serikali wenye shahada za mwanzo, za uzamivu na hata uzalimili ambao ni mbumbumbu, wajinga na wasioweza kuajirika wala kujiajiri, kutumikia taifa, hata kujitegemea.

Aidha, wanaambulia magonjwa ya ngono yanayotokana na mienendo hiyo bila kuchukua tahadhari za kujikinga na mwisho ni kupotea kwa nguvu kazi ya taifa kwani hutoka vyuoni wakiwa tayari wagonjwa na hivyo kurudi mtaani na kuanza kuumwa au mwisho kupoteza maisha wakati taifa likiwategemea.

Hili ni tatizo kubwa kwani nguvu kazi hii ambayo ni tegemeo la taifa inapotea na kufanya Tanzania kupoteza damu changa iliyokuwa inategemewa kutoa mchango katika maendeleo ya sasa na ya baadaye.

### KUDHIBITI

Ni wazi kwamba vitendo vya ngono vyuoni na shuleni ni jambo lisilovumilika katika jamii ila wanafunzi hasa wanavyuo lazima wajirekebishe na kuweka juhudi katika masomo yao na sio kukaa bila kusoma wala kufanya mazoezi ya kimasomo 'assignments' wanazopewa kwa kutegemea fadhila za maksi kutoka walimu wao.

Kwa mfano; mwanafunzi anayehudhuria darasani, anayesoma na kufanya kazi zake za mazoezi anazopewa kwa bidii, hahitaji kwenda kwa mwalimu kuomba maksi za upendeleo. Hali hii inapunguza uwezekano wa mwalimu kuonana na mwanafunzi katika muda usio wa darasa na kupunguza uwezekano wa walimu kutumia nafasi ya mwanafunzi kuomba maksi za upendeleo ili kutekeleza.

INAENDELEA UK.12

TEKNOLOJIA

NA CHRISTINA MWAKANGALE

# Teknolojia kidigitali inavyopunguza safari za nenda rudi kwenye ofisi

MABADILIKO ya teknolojia kutoka analojia kuwa digitali, yamegusa kila eneo, ingawa kuna athari chanya na hasi.

Huduma za kifedha na bima ni miongoni mwa zilizoathiriwa. Hivi sasa teknolojia mtandao, inamwezesha mteja kulipia bima iwe ya gari na afya, mifuko ya hifadhi ya kijamii bila kufuata huduma hizo ana kwa ana ofisini.

Kwenye huduma za fedha ndiko mabadiliko makubwa yameshuhudiwa, ambako ukitaka kununua au kulipia huduma yoyote huna haja ya kufika kwenye ofisi za shirika, kampuni au taasisi.




Moja ya vibanda vinavyotumika kutuma na kupokea pesa. **PICHA: MTANDAO**

Hivi karibuni wadau wa bima, fedha na wataalamu wa mifumo ya kidijitali, wanakutana Dar es Salaam, kujadili kasi na changamoto ya kiteknolojia kwenye eneo hilo na kubainisha fursa, kuelekea jubilii ya miaka 50 ya Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM).

Akiwasilisha mada kuhusu kanuni za huduma za kifedha kidijitali, chini ya mikataba ya biashara na huduma za ndani, Dk. Bill Kiwia, kutoka Ofisi ya Rais, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, anasema utafiti walioufanya karibuni unabaini kuwa hakuna maboresho ya kisheria kuendana na huduma kidigitali.

Kwenye utafiti huo, anaoshirikiana na mtafiti mwenza, Dk. Grace Kazoba, unagundua kuwa Tanzania haijaboresha sheria ya Masoko ya Mitaji na Dhamana, ili kuendana na maendeleo ya sekta ya Huduma za Kifedha za Kidijitali au kuandaa kanuni inayohusiana nayo.

> "Kwa miaka 50 ya IFM, ni matumaini yangu chuo kitawajibika katika maendeleo ya kiuchumi.

"Changamoto za teknolojia ya utoaji wa huduma za kifedha, je, sheria zetu zinawakilisha kilichoko sokoni? Uwekezaji na Usimamizi wa Mfuko wa Tanzania unasimamiwa kwa kiasi kikubwa na Sheria ya Masoko ya Mitaji na Dhamana ya 1994 sheria hiyo haifafanui mfuko bali inafafanua, miongoni mwa mambo mengine, dhamana," anasema Dk. Bill.

Anasema mchango mkuu wa utafiti huo, ni namna ukuaji wa digitali kwenye mifumo ya huduma hizo, inavyohitaji kuendana na mbinu za kisasa ili kuongeza ufanisi.

"Kwenye huduma za kifedha za kidijitali kunahitaji uwekezaji katika masuala ya mafunzo, upatikanaji wa teknolojia na mabadiliko ya mawazo ambayo yanaweza pia kuhitaji kiwango fulani cha mafunzo.

"Utafiti wetu pia umegundua kwamba maendeleo ya teknolojia ya kifedha kwa kiasi fulani yalitokana na mdororo wa kifedha duniani wa mwaka 2008 ambao uliondoa uaminifu kwa wateja."

"Kumomonyoka kwa uaminifu kulifungua njia ngumu zaidi ya kukusanya fedha kwa ajili ya biashara nchini jambo ambalo linaweza kusababisha taasisi za fedha na serikali kupoteza vyanzo muhimu vya mapato kwa mfano kuanzisha biashara," anasema Dk. Bill.

Anasema uundwaji wa soko huria la teknolojia kunaweza kusababisha upotevu wa fedha zinazohitajika zaidi kutokana na kwamba shughuli za kibiashara zinaweza kukumbana na vikwazo.

Pia anasema maboresho ya sheria zinazohusu mfumo huo, pamoja na matumizi ya tafiti zinazotolewa na wataalamu kutaleta tija, ikiwamo mapato yatokanayo na ujio wa watalii visiwani Zanzibar.

"Mfumo huu kwa nchi za nje umefanikiwa kukusanya mapato kupitia teknolojia mtandao. Tuna pengo la ukusanyaji mapato kupitia mfumo wa biashara mtandao 'e-commerce' ikiboreshwa tutakusanya zaidi," anasema Dk. Bill.

Kamishna wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA), Dk. Baghayo Saqware, akizungumza kwenye mkutano huo pia anasema, wakati matumizi ya mfumo wa bima na fedha, yakikua malengo yawekwe ya miongo mitano ijayo.

"Ipo haja ya kufanya kitu zaidi kwa miaka 50 ijayo, ikiwamo kufanya kazi pamoja hasa katika huduma zinazohusiana. Tunahusika na kusajili, kutoa na kufuta leseni pia kutoa elimu, miongozo na ushauri kwa serikali," anasema.

Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, anazungumza kwenye kusanyiko hilo, anasema mabadiliko licha ya kuchukua muda mrefu, yanafikiwa.

"Kila mara tunaambiwa Roma, haikujengwa kwa siku moja, kuna changamoto ilipitia. Kwa miaka 50 ya IFM, ni matumaini yangu chuo kitawajibika katika maendeleo ya kiuchumi.

"Kumbukumbu ya miaka hii tangu chuo kuanzishwa, ikumbukwe teknolojia ya uchumi kidigitali kama kauli mbiu inavyosema, kunahitajika uwekezaji wa viwanda, ujuzi, uzoefu," anasema Kigahe.

## Ujio madawati jinsia vyuoni uambatane na bidii, si kusubiri fadhili, maksi za bure

INATOKA UK.11

Kwanini ni muhimu kufanya hivyo? Mwanafunzi anayesoma vizuri na kufanya kazi zake vizuri hahitaji kwenda kwa mwalimu au mhadhiri ili kuomba maksi za upendeleo kwasababu kazi au mitihani yake ipo imefanywa katika kiwango kinachotakiwa na maksi zake pia zinakuwa vizuri.

Utajiuliza kuna faida gani kwa jamii kuchukua hatua hizi muhimu ? Kama kila mwanafunzi hasa mwanachuo ataweka juhudi katika kuhudhira darasani, kusoma vizuri na kufanya kazi za kimasomo wanazopewa na walimu wao tena kwa muda unaofaa itapunguza tabia ya wanafunzi kuwafuata fuata walimu ili kuomba fadhila hasa maksi za upendeleo.

Kupungua kwa tabia hii kutafanya walimu wakose nafasi ya kujiingiza kwenye uhusino wa mapenzi ili kutoa fadhila ya maksi za upendeleo kwa wanafunzi wasio stahili. Hii pia italeta faida kwa taifa kwani wahitimu watakaomaliza katika taasisi hizo watakuwa ni wale wenye sifa zinazotakiwa sio waliofaulu na kumaliza masomo yao kwa fadhila za upendeleo wa walimu wao bali ni kwa kukidhi vigezo vya ufaulu na ujuzi unaotakiwa.

Pia itaondoa dhana inayojengeka na inayozidi kujengeka kwa baadhi ya watu kuwa ili kufanya vizuri kwenye masomo ni lazima kuwa na uhusiano wa kimapenzi na walimu au wahadhiri wanaowafundisha. Dhana potofu ya kuwa hata bila kusoma kwa bidii wala kufanya kazi za darasani wanazopewa inawezekana kufaulu vizuri itakoma.

Kila mwanafunzi anatakiwa kuweka juhudi katika masomo yake ili kupunguza tabia ya kusubiri fadhila za walimu au wahadhiri ili kufaulu masomo yao. Mazoea ya kupenda fadhila za walimu ndicho chanzo kikubwa cha kuongezeka kwa vitendo vya ngono katika ya wanafunzi na walimu na wahadhiri katika taasisi nyingi za elimu ya juu.

Hii itapunguza maambukizi ya magonjwa ya zinaa na hasa virusi vya UKIMWI na VVU na mengine mengi. Tatizo ambalo limekuwa kubwa hasa katika taasisi za elimu ya juu nchini. Na zaidi vitendo hivi havikubaliki na jamii ya kitaifa na kimataifa kwa ujumla. Aidha, tabia hii ya kufaulu kwa kutegemea fadhila za walimu huzalisha wataalamu feki wasio na ujuzi wa kutosha katika fani zao na hivyo kushindwa kutoa mchango wao katika ujenzi wa taifa kama iliyotarajiwa.

Halikadhalika huondoa hali ya kujituma kwa wanafunzi wengine kwani hukata tamaa baada ya kuona wenzao ambao hawakusoma wala kufanya kazi za kimasomo wanapata ufaulu sawa au zaidi yao.

Wasomi wakumbuke wanasoma kwa kodi za Watanzania kwa maana hulipa mishahara walimu, wahadhiri, kupewa mikopo wanafunzi ili kugharamia masomo yao ili waje kutoa mchango katika ujezi wa taifa na wengine wanasoma kwa mkopo wa serikali.

ELIMU

NA JULIETH MKIRERI, KIBAHA

# Kushawishi watoto kujifelisha mitihani kunavyoimaliza Pwani

KILA mkoa unapambana kuongeza na kukuza ufaulu, lakini bado kuna kikwazo kinachosababisha kuendelea kushuka kwa elimu ambalo ni doa kwa watendaji.

Mathalani, mkoani Pwani jitihada zinafanyika kupandisha ufaulu, lakini mambo hayajakaa sawa, unashuka na zipo sababu nyingi zinazotajwa kuchangia, mojawapo ni wazazi na walezi kuwashawishi watoto wajibu mitihani vibaya ili wafeli.

Baadhi wanawashawishi kuboronga kwenye mitihani ya msingi ya mwaka 2022, yote yakisababisha mkoa kushuka kwenye viwango vya ufaulu kwa asilimia 1.174, Ofisa Elimu wa Mkoa Sara Mlaki anaeleza.

Anasema ufaulu uko chini ukilinganishwa na matokeo ya mwaka 2021, akiongeza kuwa sababu nyingine ya kushuka kwa ufaulu ni pamoja na wanafunzi wa msingi na sekondari 5,964 kuacha shule.

Sara anafafanua kuwa utoro huo umechangiwa na mimba na kati ya watoro, wanafunzi 184 walipata ujauzito.

"Suala la wanafunzi kukosa msukumo wa kujifunza kutoka kwa wazazi na walezi na hili la kutembea umbali mrefu kwenda na kurudi nyumbani linachangia mdororo kwenye ufaulu," anaeleza Mlaki.

Kutokana na hali hiyo anaeleza kuwa zipo jitihada zinazofanywa kukabiliana na vikwazo hivyo ambazo ni pamoja na kutoa tena fursa kwa wanafunzi waliokatisha masomo kutokana na sababu mbalimbali.

"Kwa mwaka 2022 wanafunzi 432 walirudi shuleni kuendelea na masomo, lakini uhamasishaji unaendelea kufanywa na viongozi kuwahimiza wazazi, walezi na wanafunzi kupenda shule," anasema.

Sara anaeleza mapendekezo ya mkoa huo kukabiliana na vikwazo hivyo kuwa ni pamoja na kuhamasisha familia kuchangia chakula cha mchana au uji kwa wanafunzi shuleni.

Aidha, kuwashirikisha wadau kujadili maendeleo na vikwazo vya watoto wao kadhalika maofisa elimu kusimamia na kufuatilia kazi za ufundishaji na ujifunzaji katika maeneo yao nacho ni kipaumbele.

Katika Wilaya ya Kisarawe inaelezwa kuwa ufaulu kwa shule za sekondari umekuwa ukishuka ukidaiwa kuchangiwa na baadhi ya wanafunzi kugoma kukaa kwenye hosteli zinazojengwa karibu na shule.



Wanafunzi kwenye chumba cha mitihani. **PICHA ZOTE: MTANDAO**



Ofisa Elimu Mkoa wa Pwani, Sara Mlaki.

Ofisa Elimu Sekondari wa Wilaya ya Kisarawe, Editha Fue, anasema serikali inafanya jitihada za kujenga hosteli karibu na shule ili kuwaondolea adha ya kutembea umbali mrefu lakini mwitikio wa jamii bado ni mdogo.

Editha anasema tabia hiyo inatajwa kuwa moja ya sababu zinazochangia kushuka kwa ufaulu katika wilaya hiyo pamoja na ukosefu wa chakula shuleni hali inayochangia wanafunzi kushindwa kumudu masoma wakiwa na njaa.

Ofisa Elimu Msingi wa Wilaya ya Kisarawe Hadija Mwinuka, anasema ipo haja ya wazazi na walezi kupatiwa kuhusiana na umuhimu wa elimu kwa watoto wao ili waweze kuwa karibu na walimu na watoto wao, lakini kuondoa tabia ya kuwashawishi kufeli kwenye mitihani yao ya kuhitimu elimu.

Anasema endapo wazazi na walimu watakuwa wanakutanishwa mara kwa mara na kujadili kwa pamoja namna ya kutatua vikwazo vilivyoko itainua ufaulu na kuwaandaa wasomi katika wilaya hiyo na mkoa.

Hata hivyo, baadhi ya wadau wa elimu wanapendekeza namna ya kukabiliana na utoro shuleni na kukuza ufaulu kwa wanafunzi kuwa ni pamoja na kushirikisha wazazi na walezi kwa kila hatua na kufanya nao mikutano ya mara kwa mara, kupanga na kutekeleza wanayokubaliana.

> Tutashuka mpaka kwenye matawi kuwaelimisha namna ya kuwalea watoto, siyo kuwaacha wakitangatanga mtaani hali ambayo inachangia kuwarudisha nyuma na kutoona umuhimu wa elimu.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi Wilaya ya Bagamoyo, Abubakar Mlawa, anapendekeza mabaraza ya madiwani kutunga sheria ndogo ndogo za kuwabana wazazi na walezi wenye watoto watoro pamoja na wale wanaopata mimba.

Mlawa anasema yapo maeneo watoto wanakatisha masomo bila sababu za msingi na wazazi hawachukulii hatua suala hilo na hivyo kuongeza idadi ya watoro huku serikali ikiendelea kuboresha mazingira za ufundishaji na kujifunzia.

"Hili linatakiwa lifanyiwe kazi kwenye halmashauri zetu, serikali inajenga vyumba vya madarasa lakini kama huu utoro tutaendelea kuunyamazia yapo maeneo vyumba vitakosa wanafunzi hili halitakiwi kunyamaziwa," anasisitiza.

Mjumbe wa Kamati ya Utekelezaji ya Jumuiya ya Wazazi (CCM) Mkoa wa Pwani, Selina Koka, anasema kutokana na hali ya kushuka kwa ufaulu wanajipanga kukutana na wazazi na walezi katika maeneo mbalimbali kujadili umuhimu wa elimu.

Selina anasema katika ziara yao wanatarajia kuwaelimisha wazazi na walezi kuhusiana na uchangiaji wa chakula shuleni kwa kuwa na utaratibu maalumu ambao hautamuumiza yeyote.

"Tutashuka mpaka kwenye matawi kuwaelimisha namna ya kuwalea watoto, siyo kuwaacha wakitangatanga mtaani hali ambayo inachangia kuwarudisha nyuma na kutoona umuhimu wa elimu," anaeleza Selina.

Kadhalika, watagusa eneo la ukatili wa kijinsia, kwa kuhakikisha kila mtoto anapata haki sawa ya elimu.

"Tutasaidiana na serikali kuhakikisha wazazi, walezi na walimu wanashirikiana na kupata chakula wakiwa shule, wasome vizuri na ufaulu uongezeke katika mkoa wetu," anasema Selina.

Mara kwa mara katika mikutano yake Mkuu wa Mkoa wa Pwani Abubakar Kunenge, amekuwa akisisitiza wazazi na walezi wa mkoa huo kusimamia suala la elimu kwa watoto wao ili waweze kunufaika na ajira kwenye viwanda vinavyojengwa katika mkoa huo.

Ngoma za vigodoro, unyago, utoro pamoja na baadhi ya watoto kulelewa na bibi zao ni moja ya vitu vinavyoelezwa kushusha ufaulu kwa mkoa huo.

ELIMU

NA MARTHA SAMBO, IRINGA

# Iringa yawa 'kuzimu' kwa watoto, taifa la kesho lawekwa hatarini

• Ubakaji wafikisha 12 hospitalini kila mwezi



Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Halima Dendego na wadau wengine wanatakiwa kufanya kazi ya ziada kunusuru watoto na unyanyasaji kingono. **PICHA: MTANDAO**

ULAWITI na ubakaji siyo tena msamiati mgeni masikioni mwa wengi, licha ya kuwa na athari nyingi za kiafya kwa watoto wa kike na wanaume.

Vitendo hivyo mbali na kuacha ulemavu wa kudumu kwa watoto na kuwaathiri kimwili, kisaikolojia, huwaachia majeraha hata ujauzito, maradhi, baadhi yao hupoteza maisha na kukosa haki ya msingi ya kuishi.

Taarifa kutoka Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Iringa, inaripoti kuwa watoto 12 kila mwezi hufikishwa hospitalini hapo ukiwa ni wastani wa watoto wawili hadi watatu kwa wiki, kesi za kubakwa na kulawitiwa.

Mganga Mfawidhi, Alfred Mwakalebela, anasema matukio ya ubakaji na ulawiti kwa watoto yanaongezeka mkoani humo, licha ya hatua mbalimbali ya kudhibiti kuchukuliwa.

Anasema Iringa ni miongoni mwa mikoa inayokabiliwa na matukio ya watoto kubakwa na kulawitiwa kwa kiwango kikubwa.

"Kesi za ubakaji katika hospitali yetu kwa wiki tunapata kati ya watoto wawili hadi watatu na kwa mwezi kesi za kubaka watoto na wanawake tunazipokea kuanzia 12, kwa hiyo ubakaji kwa Iringa ni mwingi na idadi itakuwa kubwa zaidi huko mitaani," anasema Dk. Mwakalebela.

Aidha, takwimu za Jeshi la Polisi zinaeleza kuwa mwaka 2019 matukio 15,680 ya ukatili wa kijinsia kwa watoto ukiwamo ubakaji yalirekodiwa kitaifa na kwamba matendo hayo yamekuwa yakiongezeka kila mwaka. Mathalan, 2017 polisi inasema yalikuwa 13,457 na uliofuata yakawa 14,419.

**SABABU ZA UKATILI**

Ulawiti na ubakaji unaongezeka mkoani Iringa, Mwenyekiti wa Mtaa wa Kihesa Kilolo, Kata ya Mkimbizi Manispaa ya Iringa, Omary Juma, anasema zaidi ya watoto 28 katika kata yake, wameathirika.

"Watoto takribani 30 walilawitiwa na walibakwa, kesi ziko mahakamani, tunazifuatilia na katika mtaa wangu wa Kihesa Kilolo tatizo ni kubwa Shule ya Igeleke na zinazopakana na hizo, tatizo hili ni kubwa."

"Tunashindwa kulidhibiti kwa sababu familia hazitoi ushirikiano, watoto wale wale waliobakwa wako bado kwenye mazingira magumu, wanaachwa peke yao hakuna anayewasimamia, wala anayewafuatilia, wamebaki wanafanyiwa ukatili, wameachwa huru," anaongeza.

Mwenyekiti Omary, anataja kukosa malezi sahihi ya wazazi na kutumbukia katika mikono isiyo salama kuwa ni sababu ya matukio hayo kushamiri.

"Tatizo kubwa liko kwenye malezi ya familia watoto wanajilea wenyewe, kuanzia asubuhi hajamuona mama wala baba wanatafuta maisha. Analelewa na watu wengine na mwisho wa siku ndiyo wanaotengeneza mazingira na kumbaka, wazazi na walezi hawana habari," anaongeza Omary.

Anautaja ushirikina na ukosefu wa maadili kwenye jamii ukiwamo matumizi ya dawa za kulevya na makundi rika yanayoendekeza tabia hatarishi kuwa ni chanzo.

Ripoti ya Umoja wa Mataifa kuhusu hali ya kimataifa ya kuzuia ukatili dhidi ya watoto ya mwaka 2020 inabainisha kuwa nusu ya watoto duniani sawa na takribani watoto bilioni moja kila mwaka wanaathirika na ukatili wa kimwili, kingono au kisaikolojia na kujeruhiwa.

Watoto hao husababishiwa ulemavu wa kudumu na wakati mwingine kifo kwa sababu serikali zinashindwa kufuata mikakati iliyowekwa ya kuwalinda watoto.

Ripoti iliyopewa jina la "hali ya kimataifa katika kuzuia ukatili dhidi ya watoto 2020" ni ya kwanza ya aina yake ikiainisha hatua zilizopigwa katika nchi 115 chini ya mkakati wa INSPIRE ambao unajumuisha mikakati saba kuzuia na kukabiliana na ukatili dhidi ya watoto.

Karibu nchi zote zina sheria muhimu za kuwalinda watoto dhidi ya ukatili lakini ni chini ya nusu ya nchi hizo mikakati hiyo inatekelezwa ipasavyo.

**ATHARI**

Paskalina Lweve, Diwani wa Viti Maalumu Manispaa ya Iringa, anaeleza kuwa madhara ya ubakaji na ulawiti ni endelevu hata wakiwa wakubwa, hivyo hatua za haraka zinahitajika kuwalinda watoto.

"Watoto wetu watakuwa katika wakati mgumu kwa sababu tutajua tuko na watoto wa kiume kumbe wameshaharibika, sijui niseme ni wanawake au sijui niseme ni nini kwa sababu kitakuwa ni kizazi kilichoharibikiwa ni majanga makubwa, tusifumbie macho kuna madhara kwa nguvu kazi ya taifa," anasema Paskalina.

Peter Mkwama ni Mwenyekiti wa Baraza la Wazee na Ushauri Mkoa wa Iringa, anasema matokeo ya kushamiri kwa vitendo vya ubakaji na ulawiti katika jamii ni kupuuzia maonyo ya wazee hasa yanayohamasisha kujenga jamii yenye maadili na haki.

Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009, inaeleza kuwa jamii ina wajibu wa kuwalinda watoto dhidi ya hatari zote hasa inayohatarisha usalama na mstakabali wa maisha yao.

Kwa mujibu wa sheria hiyo, endapo mtu atafanya vitendo vinavyoharibu utu wa watoto atakabiliwa na adhabu kikiwamo kifungo.

Ikiwa jamii na familia wakizungumza na watoto na vijana wa rika balehe kuhusu madhara ya matukio hayo, huenda ikasaidia kutokomeza ukatili huo.

"Lazima, tuzungumze na familia, turudi kwa vijana wetu, tunakazana kuzungumza na watoto wetu huku vyanzo ambavyo ni familia tukiviacha, haiwezekani hadi mtoto mchanga abakwe na kulawitiwa huku kwetu mtoto amelawitiwa hadi wa miaka mitatu, wazazi na jamii iko wapi? Lazima tulitazame hili haiwezekani," anasema Mkwama.

Viongozi wa dini nao wana nafasi kubwa katika mapambano dhidi ya ubakaji na ulawiti, kwa lugha nyingine ndiyo wana nafasi kuhakikisha matendo maovu kama ulawiti na ubakaji mkoani Iringa vinakoma.

"Lazima tufike mahali serikali, wadau mbalimbali na sisi viongozi wa dini tuweke nguvu ya pamoja kukabiliana na vitendo hivyo ili kuvitokomeza huku tukiendelea kutoa elimu juu ya madhara ya ukatili dhidi ya watoto."

**UDHIBITI**

Kutokana na ukubwa wa tatizo Manispaa ya Iringa imeanzisha kampeni ya kutokomeza ukatili kwa kushirikiana na viongozi wa dini.

Ibrahimu Ng'wada ni Meya wa Manispaa ya Iringa anayesema wamebaini uwepo wa utitiri wa matukio ya ubakaji na ulawiti kwa watoto.

"Sisi halmashauri tuliitisha mkutano kwa viongozi wa dini zote, ili tusaidiane kutoa elimu kwa wananchi lakini na wao walikuja na mapendekezo kuwa ianzishwa siku maalumu ya kuadhimisha kupinga ukatili wa kijinsia mkoani humo," anasema Ng'wada.

Jane Mwalembe ni Mkurugenzi wa Taasisi ya Kupambana na Ukatili anasema kupaza sauti na kukemea vitendo hivyo kupunguza wahalifu kukamatwa na matukio hayo kupungua kwenye jamii.

Kwa mujibu wa taarifa ya Mahakama Kuu Kanda ya Iringa kesi za ubakaji mkoa humo, wamezidi kuongezeka na zinapewa kipaumbele na kuwatia hatiani wanaobainika kutenda makosa hayo ya ukatili.

Kesi hizo ni ubakaji Wilaya ya Iringa 35, Kilolo 19 na Mufindi kwa kipindi cha Januari hadi Septemba mwaka 2022.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Iringa, Sunday Songwe, anasema jeshi hilo linaendelea na misako ili kudhibiti uhalifu huo, akiwataka wananchi kutoa taarifa za uwepo na viashiria vya ukatili mkoani humo.

"Tunapambana na uhalifu na wahalifu wa ubakaji na ulawiti kwa kuwafikisha mahakamani watuhumiwa ili sheria ifuate mkondo wake. Niwaombe wananchi tushiriki kikamilifu kutoa taarifa na si kuliachia Jeshi la polisi pekee," anasema Songwe.

Baadhi ya wazazi na walezi katika Manispaa ya Iringa wanakiri wazi uzembe wao unachagiza kuongezeka kwa matukio hayo na kwamba wamepata funzo kusimama vema katika jukumu lao la malezi ya watoto.





## Kesi aliyekuwa Katibu Anglikana, Baraza Wadhamini yapigwa kalenda

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KESI ya aliyekuwa Katibu Mkuu wa Kanisa la Aglikana Tanzania, Dk. Mecka Ogunde, dhidi ya Baraza la Wadhamini wa Kanisa hilo iliyofunguliwa na Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA) Dodoma imepigwa kalenda hadi Februari 6, mwaka huu.

Hatua hiyo inakuja baada ya msuluhishi aliyepaswa kusikiliza shauri hilo namba CMA/DOM/84/2022, kupata udhuru hali iliyosababisha kuahirisha.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi baada ya kuahirishwa kwa shauari hilo, Wakili Willison Ogunde, alisema shauri lao la mgogoro wa kikazi baina ya Dk. Ogunde dhidi ya Baraza la Wadhamini wa Kanisa Aglikana Tanzania lilipaswa kusikilizwa juzi.

"Kama ilivyoamuliwa na Mahakama Kuu ya Dodoma Desemba 27, mwaka jana chini ya Jaji Masaju alipotupilia mbali maombi ya marejeo yaliyowasilishwa kule na wadhamini wa Kanisa la Aglikana Tanzania, CMA ikawa imetupangia kuja leo (juzi) kuendelea kusikilizwa lakini msuluhishi aliyepaswa kusikiliza shauri hili hakuwapo hivyo kuahirishwa hadi Februari 6, mwaka huu," alisema Wakili Ogunde.

Aidha, alisema Mahakama Kuu Kanda ya Dodoma, ilitupilia mbali maombi ya Baraza la Wadhamini wa Kanisa hilo kupinga Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA) Mkoa wa Dodoma kuendelea kusikiliza mgogoro huo wa kikazi nje ya muda.

"Lakini Mahakama Kuu iliamua kuwa CMA, ilitenda haki na ilifuata sheria kwa kuruhusu mgogoro huu wa kikazi baina ya Dk. Ogunde na Baraza la Wadhamini wa Kanisa Aglikana Tanzania uendele kusikilizwa na leo CMA ilitupangia kuja kwa ajili ya kuendelea na usikilizwaji wa mgogoro huu,"alisema.

Naye wakili wa mlalamikiwa Sostenes Mseligwa, alisema juzi ilikuwa siku ya kutajwa kwa shauri hilo lakini tayari wamepeleka maombi yao ya kupeleka shauri hilo Mahakama ya Rufani.

Julai 27, mwaka jana Wakili Ogunde akizungumza na waandishi wa habari alisema wamefikia maamuzi hayo baada ya Baraza la Wadhamini wa Kanisa Anglikana Tanzania, kushindwa kufika makubaliano na mteja wake.

# Bunge lakoshwa na uamuzi TRA kutotumia kikosi kukusanya

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Uwekezaji na Mitaji ya Umma (PIC), imesema uamuzi wa serikali kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) wa kutotumia kikosi kazi kwenye kukusanya kodi kumeongeza makusanyo na kupunguza matumizi ya taasisi hiyo.

Akizungumza jana baada ya kukutana na TRA, Wakala wa Viwango Tanzania (TBS) na Wakala wa Ufundi na Umeme nchini(TEMESA), Mwenyekiti wa kamati hiyo, Jerry Silaa, alisema kamati inampongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuagiza kodi zikusanywe bila kutumia nguvu.

"Tunampongeza Rais mtakumbuka alivyoingia madarakani aliagiza kodi zikusanywe bila kutumia nguvu, ametoa kibali cha ajira zaidi ya maofisa 2,000, watasaidia ufanisi wa taasisi, nini kimetokea ukiangalia katika mwaka wa fedha 2022/23, TRA iliweka lengo la kukusanya Sh.trilioni 23.6 ikilinganishwa na makusanyo halisi ya mwaka jana 2021/22 ya Sh. trilioni 20.9."

"Hadi kufikia Desemba 2022 TRA ilishakusanya Sh.trilioni 11.1 sawa na asilimia 98.1 ya lengo, ukiangalia miaka ya nyumba 2017/18 walifikia lengo kwa asilimia 86, mwaka 2019/20 walifikia kwa asilimia 92, mwaka 2020/21 walifikia lengo kwa asilimia 87,"alisema.

Silaa alisema kwenye taarifa ya utendaji kazi ya mwaka 2022/23 ambayo TRA inakusanya kodi kwa ridhaa na bila kutumia nguvu kwa wafanyabiashara, imefikia lengo la asilimia 98.1.

Aidha, alisema kwa mwaka 2020/21 matumizi ya TRA yalikuwa juu kulikosababishwa na posho za kikosi kazi cha kukusanya kodi.

"Baada ya kuondoa kikosi kazi siyo tu makusanyo yameboreka lakini matumizi ya taasisi yamepungua, tunapongeza serikali na TRA ya kuona maamuzi ya kutotumia nguvu na mabavu kwenye kukusanya kodi kwa kuwa ni suala la kitaalamu,"alisema.

Kuhusu TBS, Silaa alisema mwaka jana Bunge lilifanya maamuzi ya kuitaka TBS ihusishwe na kazi ya kuweka vinasaba kwenye mafuta.

"Awali kazi hii ilikuwa inafanywa na kampuni binafsi na kama mtakumbuka ilileta mjadala mkali pale bungeni na tuliamua kwa pamoja kuwa TBS kama taasisi ya serikali ifanye hii kazi, nia ni kupunguza gharama lakini kutengeneza taasisi yenye uzalendo, wakati ule ilikuwa ni Sh.14 kwa lita lakini TBS wanatoza gharama ya Shilingi nane kwa lita na wanaelekea kufika Shilingi saba kwa lita,"alisema.

Alisema vinasaba hivyo hununuliwa nje ya nchi lakini TBS imeijulisha kamati ipo kwenye mchakato wa kuanza kutengeneza hapa nchini.

Akizungumzia kuhusu TEMESA Silaa alisema kamati imeagiza taasisi za serikali zinazodaiwa na wakala huo kulipa madeni yake ambayo yamefikia zaidi ya Sh.bilioni 44.



Mtendaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania, Prof. Elisante Ole Gabriel, akizungumza na wafanyakazi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi alipotembelea banda la tume hiyo kwenye maonesho ya Wiki ya Sheria viwanja vya Nyerere Square jijini Dodoma jana. **PICHA IBRAHIM JOSEPH**

## W'biashara watakiwa kupima afya kuwakinga wateja na magonjwa

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

WAFANYABIASHARA wa chakula wametakiwa kupima afya zao ili kuwakinga wateja na magonjwa ya kuambukiza.

Rai hiyo ilitolewa na Mganga Mkuu wa Jiji la Dodoma, Dk. Andrew Method, wakati akifungua mafunzo ya siku moja kwa watoa huduma za afya ngazi ya kata yaliyofanyika mwisho wa wiki jijini hapo kwa uratibu wa Shirika la Amref.

Dk.Method aliwataka wafanyabiashara wa huduma ya chakula kuzingatia kupima afya zao ili kuwakinga wateja wao na magonjwa ambukizi.

"Najua hapa kuna watendaji na wasimamizi wa huduma za afya kwa kata zote za Jiji hivyo nawataka mkasimamie suala la kuhakikisha watoa huduma ya chakula katika maeneo yote wapime afya zao ili kuepusha magonjwa ya kuambukiza," alisema.

Alieleza kuwa sheria inawataka watoa huduma zote za chakula kupima afya kabla ya kufungua biashara, lakini utekelezaji umekuwa ukikiukwa na baadhi ya watu.

Alibainisha kuwa mafunzo hayo yamewakutanisha watu ambao ni wasimamizi wa sheria katika maeneo hayo, hivyo wazingatie kusimamia sheria katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku.

Aidha, alihimiza kusimamia usafi wa mazingira kwenye maeneo yao ili kuzuia magonjwa yanayosababishwa na uchafu, huku akidai kuwa Jiji hilo litakuwa na mpango wa kushindanisha kata zote kuhusu usafi na washindi watapata zawadi mbalimbali.

Meneja Mradi wa Maji na Usafi wa Mazingira kutoka AMREF, Mhandisi Mturi James, alisema lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo wa kazi ili jamii kuendelea na kujikinga na ugonjwa wa corona pamoja na magonjwa mengine ya kuambukiza.

Mhandisi James alisema mradi huo unatekelezwa katika Mkoa wa Dodoma kwa Halmashauri ya Jiji la Dodoma na Mwanza na unatekelezwa kwa zaidi ya Sh.milioni 100.

Alisema mradi huo unatekelezwa kwa kuwawekea vifaa vya kunawa pamoja na miundombinu ya maji kwa baadhi ya maeneo ya umma na shule.

Alibainisha kuwa lengo la mradi ni kuwafikia watu zaidi ya milioni moja kwa maeneo hayo ya utekelezaji wa mradi huo.

Ofisa Mradi wa AMREF, Mhandisi Agapiti Shayo, alisema mradi huo kwa Mkoa wa Dodoma unatekelezwa katika Halmashauri ya Jiji na utazifikia shule 10 na vituo 10 kwa kuwezeshwa vifaa vya kunawa mikono na miundombinu ya maji kwa maeneo ambayo hayana.

Alisema katika eneo hilo wanatarajia kugawa vifaa vya kunawa mikono 5,000 ngazi ya jamii kwa halmashauri hiyo kwa kata 41.



# Watu saba mbaroni tuhuma za mauaji Hakimu Mkazi

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

JESHI la Polisi mkoani Mbeya linawashikilia watu saba kwa tuhuma za kuwaua watu wawili akiwamo Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Wilaya ya Handeni mkoani Tanga, Joachim Mwakyolo (51) na mwenzake ambaye jina lake bado halijafahamika.

Watu hao wanadaiwa kutekeleza mauaji hayo kwa kuwapiga mawe kisha kuwakata na vitu vyenye ncha kali kichwani na mikononi kwa kile kinachodaiwa kuwa walikuwa wanagombea mashamba.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, Benjamin Kuzaga, alisema tukio hilo lilitokea Januari 20, mwaka huu, katika Kijiji cha Kibole kilichoko Kata ya Itete katika Halmashauri ya Busokelo.

Aliwataja watuhumiwa waliokamatwa kuwa ni Amokile Mwakangundya (30), Zawadi Mwakagile (27), Lutengano Mwakagile (27), Wito Mwakatobe (19), Lwitiko Kikomile (27) na Tubike Kisasa (48) wote wakazi wa Kijiji cha Kibole pamoja na Aliko Mwakikyoko (40) Mkazi wa Kijiji cha Ngichwa wilayani Kyela.

Alisema hakimu huyo alikuwa na mgogoro wa ardhi na Serikali ya Kijiji hicho ambao ulisababisha wapelekane katika mahakama mbalimbali kwa ajili ya usuluhishi.

"Serikali ya kijiji inadai eneo hilo ni hifadhi ya msitu lakini hakimu huyo alikuwa anadai ni eneo lake ambalo alilinunua kwa mmoja wa wenyeji wa kijiji hicho, walipelekana mahakamani na kesi yao ilikuwa inafikia ngazi ya mahakama kuu," alisema Kamanda Kuzaga.

Alisema kesi hiyo ilianza mwaka 2018 lakini mwaka 2021 ilikamilika katika Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Mbeya ambapo hukumu ilionyesha kuwa wanakijiji hao walikuwa wamepata ushindi dhidi ya marehemu. Alisema Januari 20 saa 2:00 usiku mwaka huu marehemu pamoja na mwenzake walionekana wakipita katika eneo la mgogoro jambo ambalo liliwashtua wanakijiji.

Alisema baadhi ya wananchi wa kijiji hicho waliokuwa kilabuni waliwasimamisha na kuanza kuwahoji sababu zilizowafanya wapite kwenye eneo hilo wakati hawaruhusiwi.

Alisema wakati wanaendelea kuhojiana ziliibuka vurugu zilizosababisha hakimu huyo kuwafyatulia risasi wananchi waliokuwa wakimzonga na kuwajeruhi wawili kwenye maeneo mbalimbali ya miili yao.

Alisema hakimu huyo alijeruhi watu wawili ambao ni Tubuke Kisasa (48) ambaye alijeruhiwa sehemu ya paja la mguu wa kulia na Huruma Mwakakigura (45) ambaye alijeruhiwa kwenye ugoko wa mguu wa kulia.

"Baada ya wawili hao kujeruhiwa ndipo kundi kubwa la wananchi liliibuka na kuanza kumshambulia Hakimu Mwakyolo na mwenzake mpaka kusababisha mauaji hayo," alisema Kamanda Kuzaga.

Kamanda Kuzaga alisema baada ya kupata taarifa hizo, makachero wa Jeshi la Polisi walifika katika eneo la tukio ambapo walikuta mawe yaliyotumika kuwashambulia marehemu pamoja na silaha aliyokuwa nayo marehemu ikiwa na magazine mbili ambazo zote hazina risasi.

Alisema watuhumiwa wamekamatwa, wapo mahabusu wakiendelea kuhojiwa wakati wengine wakiendelea kusakwa kwa ajili ya hatua zaidi za kisheria.

Aliwataka wananchi mkoani Mbeya kuacha tabia ya kujichukulia sheria mkononi kwa maelezo kuwa ni kinyume cha sheria za nchi na kwamba wakikamatwa wataendelea kuchukuliwa hatua kali.



Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Rashid Chuachua (kushoto) na Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi wa Polisi, Benjamin Kuzaga, wakifyeka nyasi kandokando ya barabara ya Mahakama Kuu jijini humo mwishoni mwa wiki, wakati wa uzinduzi wa ufanyaji usafi utakaokuwa unafanywa na polisi kila mwezi. **PICHA: NEBART MSOKWA.**

## RC abaini mawakala kufanya hujuma mbolea ya kukuzia

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera amefanya ukaguzi wa mbolea kwenye maghala mbalimbali ya kuhifadhia katika Jiji la Mbeya na kubaini kuwa baadhi ya mawakala wakifanya hujuma.

Homera alifanya ziara hiyo mwishoni mwa wiki akiwa ameambatana na baadhi ya maofisa wakiwamo wa idara ya kilimo ambao katika ukaguzi waliofanya walikuta wananchi wakihaha kutafuta mbolea huku zikiwa zimefungiwa na mawakala.

Homera alisema aliamua kufanya ukaguzi huo baada ya kupokea malalamiko ya wananchi wakidai kuwa mbolea za kukuzia zimeadimika madukani katika kipindi ambacho zinahitajika zaidi na wakulima kuliko za kupandia.

Alisema walipofanya ukaguzi huo walibaini kuwa mbolea za kupandia ndizo zilikuwa zinauzwa na mawakala, huku za kukuzia zikiwa hazionekani lakini wakabaini kwamba zilikuwa zimefichwa.

"Tumebaini kuwa hawa mawakala wamezificha mbolea hizi kwenye maghala na hawazisambazi kwa wakulima, sasa wakiendelea na hujuma hizi tutawachukulia hatua kali sana za kisheria," alisema Homera.

Hivyo, aliwataka mawakala wote kuhakikisha wanasambaza mbolea kwa wakulima ili kutimiza lengo la serikali la kuhakikisha bidhaa hizo zinawafikia wakulima kwa wakati na kuongeza tija kwenye uzalishaji.

Baadhi ya wakulima walisema mbolea hizo za kukuzia ndizo wanazihitaji zaidi kwa sasa kutokana na mazao mengi kuhitaji kukuziwa na machache kuhitaji mbolea za kupandia.

# DC afichua mbinu mpya ya mahakimu kupokea rushwa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKUU wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Rashid Chuachua, amesema baadhi ya mahakimu na majaji mkoani Mbeya wamebuni mbinu mpya ya kupokea rushwa kwa kutumia miamala ya simu zisizokuwa zao ili kuficha utambulisho wao pale wanafuatiliwa na vyombo vya dola.

Alifichua mbinu hiyo wakati wa maadhimisho ya Wiki ya Sheria nchini, ambayo kimkoa yalifanyika katika viwanja vya Kabwe jijini Mbeya.

Dk. Chuachua alisema amepokea malalamiko mengi ya wananchi wakiwalalamikia baadhi ya mahakimu na majaji kwa vitendo vya rushwa.

Alisema kila akifuatilia malalamiko hayo ya wananchi hubaini kuwa watumishi hao wa mahakama hupokea rushwa hiyo kwa miamala ya simu zisizokuwa za kwao ili wasibainike.

"Changamoto kubwa tuliyonayo ni kwamba hatuna mamlaka ya kuingilia mfumo wa mahakama, lakini niseme tu hapa, kwamba upo utaratibu wa mahakimu kuomba rushwa kwa kutoa namba za miamala ya simu zisizo zao, sio rahisi kuwakamata kwa kutumia miamala ya simu," alisema Dk. Chuachua.

Alisema kuwa wananchi wanafika kulalamika wakiwa tayari wametoa fedha kupitia miamala ya simu, lakini unapofuatilia miamala hiyo unakuta simu hizo sio za mahakimu.

Aliitaka Mahakama ya Tanzania kufuatilia na kukomesha vitendo hivyo miongoni mwa watumishi wa mahakama ili kuhakikisha wananchi wanapata haki wanazostahili.

Akizungumzia mbinu hiyo, Naibu Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, (TAKUKURU) Mkoa wa Mbeya, Vaksela Malimoto, alikemea vitendo hivyo kwa kusema kuwa vitendo hivyo ni kinyume cha sheria na kwamba taasisi hiyo inao uwezo wa kufuatilia na kuvikomesha.

Alisema kuwa endapo hakimu au jaji atathibitika kufanya vitendo hivyo atakuwa pia amefanya kosa lingine la uhujumu uchumi na utakatishaji wa fedha.

Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu Kanda ya Mbeya, Rose Ebrahim, alisema kuwa Mahakama inachukua kero hiyo na inakwenda kufanyiwa kazi.

Alisema kuwa kupitia vikao vyao vya ndani watachunguzana, kukemeana na ikiwezekana kuwajibishana pale watakapobaini kuwa miongoni mwao kuna watumishi wanafanya vitendo hivyo.

Baadhi ya wadau wa sheria walisema kauli mbiu ya wiki ya sheria mwaka huu, inayosema 'Umuhimu wa utatuzi wa migogoro kwa njia ya usuluhishi katika kukuza uchumi endelevu ni nzuri na imekuja katika muda muafaka.

Hata hivyo Jaji Kiongozi wa Mahakama Kuu iliiomba TAKUKURU kufanya uchunguzi wa tuhuma hizo za rushwa zilizoibuliwa ili hatua zichukuliwe endapo itathibitika kuwa ni kweli.



# DK. Mwinyi: Watendaji tekelezeni maagizo ya serikali kwa wakati

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi amewataka watendaji wa taasisi za umma kutekeleza kwa wakati maagizo yanayotolewa na serikali ili kujenga ufanisi wa majukumu yao.

Alitoa agizo hilo jana wakati akifungua mkutano wa tano wa Baraza la Taifa la Biashara, Ikulu, Zanzibar.

Alisema ameunda Taasisi ya Ofisi ya Rais ya Ufuatiliaji na Usimamizi wa Utendaji Serikalini (PDB) ili ifuatilie mambo yote yanayoamuliwa na serikali kwa nia ya kuyapatia suluhisho kwa wakati.

"Nimeunda taasisi hii lengo ni kufuatilia utekelezaji wa mambo yote tunayoyaamua serikalini," alisema Dk. Mwinyi.

Alisema uchumi wa Zanzibar unakabiliwa na matatizo mbalimbali licha ya kuendelea kuimarika na kueleza kuwa baadhi ya matatizo hayo yako ndani ya uwezo wa serikali kwa ajili ya kuzitatua na baadhi yao ziko nje ya uwezo kutokana na sababu za kiulimwengu.

Rais Dk. Mwinyi alisema, athari za ugonjwa wa corona ziliathiri uchumi wa dunia na mataifa mengi kutetereka kiuchumi haswa uchumi wa nchi za visiwa ikiwamo Zanzibar.

Alisema licha ya ugonjwa huo kupungua na kumalizika kwa baadhi ya mataifa lakini bado umeendelea kuyaandama mataifa mengine ikiwamo China ambaye ni mshirika mkubwa wa maendeleo kwa uchumi wa Zanzibar.

Alisema sekta ya usafirishaji bidhaa ni moja ya tatizo linalohujumu uchumi wa dunia kutokana na sababu za kidunia na kueleza kuwa Zanzibar imeathiriwa na changamoto hiyo mbali na ufinyu wa Bandari ya Malindi, unaodhorotesha huduma kwenye eneo hilo.

Aidha, alisema Zanzibar kwa sasa inahitaji bandari yenye kukidhi haja zote ikiwamo bandari ya makontena, bandari ya mafuta, bandari ya samaki na bandari itakayotoa huduma za kubeba mizigo ya nafaka ikiwamo mchele yenye uhitaji mkubwa.

Alisema serikali imefanya uamuzi wa ujenzi wa Bandari ya Mangwapwani kutokana na kukidhi kwa eneo kwa ajili ya mahitaji yote pia alieleza kina kirefu cha bahari kwa eneo hilo kinakidhi haja ya ujenzi na kuongeza kuwa Mpigaduri.

Akiwasilisha taarifa ya Kamati za Baraza la Taifa la Biashara, Katibu wa Baraza hilo ambaye ni Katibu Kiongozi wa Baraza la Mapinduzi, Mhandisi Zena Ahmed Said alisema baraza lina kamati nne ambazo ni Kamati ya Uchumi na Biashara, Uwekezaji na Kulipa kodi, Kamati ya Kilimo Ufugaji, Uvuvi na Mazingira, Kamati ya Utalii na Kamati ya masuala ya Ardhi.

Mhandisi Zena alisema baraza lilifanikiwa kuzifanyia kazi kwa kuzipatia ufumbuzi hoja mbalimbali zilizowasilishwa na kamati hizo ikiwamo maslahi ya wanaopoteza ajira kwenye taasisi binafsi, udhibiti wa wanaotembeza watalii wasiorasmi, udhibiti wa nyumba za kulala wageni, maegesho ya magari yanayotumia VAT, athari za michezo ya baharini na madai ya wakulima wa mboga kwa uchelewashwaji wa madeni yao kwa taasisi za serikali.

Aidha, Mhandisi Zena alisema baadhi ya mafanikio yaliyotokana baada ya kufanyiwa kazi kwa hoja za kamati hizo ni kuanzishiwa kwa fao la ukosefu wa ajira kupitia marekebisho ya Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii, (ZSSF) Namba 5 ya mwaka 2005 na kutungwa kwa Sheria ya Mfuko wa Huduma za Afya.



Mrajisi wa Asasi za Kiraia Zanzibar, Ahmed Abdulla, akimkabidhi zawadi mmoja wa wanafunzi wa Shule ya St. Paul Kiungani wakati wa ugawaji wa taulo za kike kwa wanafunzi zilizotolewa na Taasisi ya Women and Children Support Association (WCWSA) kwa kushirikiana na wadau wengine shuleni hapo jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# TAMWA yataka kasi udhibiti matukio udhalilishaji kijinsia

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

CHAMA cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania, (TAMWA) Zanzibar, kimeitaka serikali kuongeza juhudi katika kusimamia matukio ya udhalilishaji wa kijinsia (GBV) ili haki kutendeka na kwa wakati muafaka.

Akizungumza jana na waandishi wa habari, Mkurugenzi wa TAMWA, Dk. Mzuri Issa, alisema licha ya vitendo hivyo kupigwa bado vinaendelea na kiwango cha upatikanaji wa haki bado ni mdogo.

Alisema kwa mujibu wa taarifa kutoka Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar matukio ya udhalilishaji yalioripotiwa kwa mwaka 2022 imetaja matukio 1,360 yameripotiwa katika vituo vya polisi.

Alisema inasikitisha kuona makosa yaliotiwa hatiani ni machache ambayo ni 181 sawa na asilimia 13 wakati makosa mengi bado yapo katika hatua za polisi na mahakamani.

Aidha, alisema kuna umuhimu mkubwa wa kuzidisha nguvu katika kusimamia matukio hayo katika hatua zote ili haki ya utafutaji wa haki kwa waathirika kutendeka.

Alisema watoto ndiyo waathirika zaidi wa matukio hayo hivyo, kupatikana kwa haki ni vyema waathirika kupatiwa kiwango cha kutosha cha msaada wa kisaikolojia.

# 'Wazazi msifumbie makuzi, afya ya uzazi kwa watoto'

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZAZI wametakiwa kutofumbia macho elimu ya kujitambua, makuzi na afya ya uzazi kwa watoto wao ili kuwalinda na matatizo yanayojitokeza katika jamii.

Hayo yalisemwa jana na Mrajisi wa Asasi za Kiraia Zanzibar, Ahmed Abdallah, wakati akizindua zoezi la ugawaji wa taulo za kike na elimu ya hedhi salama kwa wanafunzi wa Shule ya St. Paul na St. Monica.

Alisema kuwa ukimya uliopo kwa baadhi ya wazazi juu ya masuala ya mabadiliko ya kimaumbile ya watoto wao, husababisha madhara yakiwamo ya kiafya jambo linaloweza kudhibitiwa kwa kujenga ukaribu na kuwapa elimu kulingana na umri na nafasi ya mtoto.

Aidha, alipongeza juhudi zinazochukuliwa na asasi za kiraia ikiwamo ya WCWSA, HHFna WAJAMAMA kwa kutoa elimu inayohusu hedhi salama na kugawa taulo hizo kwa wanafunzi jambo litakaloongeza ufanisi wao katika masomo.

Alisema kuwa Serikali ya Zanzibar inathamini mchango unaotolewa na asasi za kiraia ambao unaziba pengo la kiutekelezaji wa majukumu ya serikali na kuzitaka kufanya kazi kulingana na malengo ya kuanzishwa kwao na mahitaji ya jamii.

Katibu wa Kanisa la Anglikana Zanzibar, Padri Stanley Lichinga, alipongeza usimamizi na ufuatiliaji unaofanywa na ofisi ya mrajisi kwa mashirika yasiyo ya kiserikali akisema yana msaada mkubwa kwa jamii.

Aidha, aliitaka jamii hasa wanaume kuwa karibu na watoto wao wa kike, kuwasikiliza na kuwapa njia za kujilinda dhidi ya matatizo yaliyoko katika jamii.

Ofisa Miradi wa WCWSA, Ester Mwakarobo, alisema kuwa zoezi hilo ni endelevu na kwamba litafanyika katika shule zingine za Unguja na pemba.

Alisema katika mpango kazi wa shirika hilo, mbali ya kutoa elimu ya hedhi salama na kugawa taulo za kike, pia lina mpango wa kusaidia upatikanaji wa huduma muhimu katika shule zikiwamo za maji safi na salama na chakula kwa wanafunzi.

Mwenyekiti wa HHF, Florence Robert, aliahidi kuwa wataendelea kutoa elimu juu ya usafi na hedhi salama kwa wasichana na wanawake ili kuwa na jamii salama dhidi ya maradhi yanayotokana na afya ya uzazi.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA VYETI



**NEEMA SELEMANI** anatangaza kupotelewa na vyeti,cha kidato cha nne chenye index namba **P0253-0005** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya **GREEN BIRD GIRLS HIGH** mwaka **2014**, na cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S0253-0514** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya **GREEN BIRD GIRLS HIGH** mwaka **2017**, yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
Polisi taarifa **DAR/KIJ/RB/29977/2023**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**ANTHONY HENDRY LASWAI**
Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T138 ACL TOYOTA LANDCRUISER** .
Chasses Namba
**L J710002579**, Engine Namba **1KZ0224143**
Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi .
Polisi Taarifa :
**KIL/MOS/RB/475308/2022**

**FORM 58**
**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE**
**AT ONE STOP CENTRE**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 1153 OF 2022**
**In the matter of the Estate of the late**
**JULIANA MAZIKU MALIWANGA**
**And**
**In the matter of Application for letters of Administration**
by
HAWA LUMELEZI

**GENERAL CITATION**
(Rule 75)

**All persons** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the **06 day of 02, 2023**
Dated at DAR ES SALAAM this **13 day of 12, 2022**

Senior Resident Magistrate

## KUPOTEA KWA NYARAKA YA KIWANJA

**Peter Kiyabo Kapingu**
anatangaza kupotelewa na nyaraka ya umiliki wa kiwanja namb**a 335 kitalu "EE"** kilichopo Ngokolo Manispaa ya Shinyanga.
Kwa yeyote atakaiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilichopo karibu au awasiliane na Peter Kiyabo Kapingu kwa simu namba **0754-277971**
**Taarifa ya Polisi**
**SHI/SHI/RB/30727/2023.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO**
**WILAYA YA MOROGORO**
**MKOA WA MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi Na......09/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU: MARIA MDENG'O WA KONGA STREET**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA: JOYCE AKU MZENA**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 24 Mwezi 1 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**

- Wosia wa marehemu huyo upo mahakaman na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia wowote.

**Imetolewa leo tarehe 20 mwezi 1 mwaka 2023**

**HAKIMU MFAWIDHI**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**TONNY WILSON MALLE**
anatangaza kupotelewa kwa kadi ya gari aina ya **VOLKS WAGEN MALLE yenye** usajili namba: **T696 BMN, CHASSIS NAMBA: WVWZZZ1JZXP116246 na ENGINE NAMBA: AGN00AZ.**
Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA: ARU/ARU/RB/31689/2023**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO**
**WILAYA YA MOROGORO**
**MKOA WA MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi Na......10/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU: SWEDI KIGUNGULI WA MAGURUMBASI**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA: TWAHA SWEDI KIGUNGULI**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 30 Mwezi 1 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**

- Wosia wa marehemu huyo upo mahakaman na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia wowote.

Imetolewa leo tarehe 22 mwezi 1 mwaka 2023

**HAKIMU MFAWIDHI**

**FOMU YA MIRATHI-2**
**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo Wilaya MOROGORO**
**Kituo cha MJINI**
**Mkoa wa MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi Na. 02/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHENU**
**HADIJA ALLY KILIA WA AZIMIO**
**KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA**
**MOHAMED ABDALLAH MNEKA**
**TANGAZO**
(Kanunu ya 5 (2) kanuni za usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 03/ Mwezi 02 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Zingatia;
Endapo kuna yeyeto mwenye Wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.

- * Wosia wa Marehemu huyu upo Mahakamani na waweza kukaguliwa
- * Marehemu hakuacha wosia
- * Futa isiyohusika

**Imetolewa leo tarehe 06 mwezi 01 mwaka 2023**

HAKIMU MAHAKAMA YA MWANZO MJINI MOROGORO

## KUPOTEA KWA VYETI



**NDG.MASUBI J.KATENGA**
Anatangaza kupotelewa na cheti chake cha kidato cha Nne (IV),chenye Index na.S0423-0083 (CSEE),kilichotolewa na Baraza la mitihani Taifa,kupitia shule ya sekondari Bulima,iliyopo mkoa wa Simiyu.

Kwa yeyote atakayekiona anaombwa kuripoti kwenye kituo chochote cha polisi kilicho karibu.
**TAARIFA YA POLISI: NY/RB/446/2022**

**IN THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**THE REGISTRATION OF DOCUMENTS ACT (Cap. 117 R.E. 2002)**
**CHANGE OF NAMES BY DEED POLL**

THIS DEED POLL is made this of 16th day of January, 2023.
By THIS DEED POLL, I, the undersigned and the person, with the names ERNESTER BARTHOLOME KIMARIO, a resident of Kawe Beach Kinondoni District, Dar es salaam City, a Citizen of the United Republic of Tanzania by birth DO HEREBY ABSOLUTELY and utterly renounce, relinquish and abandon the use of my former names of AMBROSIA BARTHOLOME KIMARYO as variably used on my Public Pension Fund (PPF) with membership card number 67310 so as to adopt the name of ERNESTER BARTHOLOME KIMARIO that appeared on my Citizen Identity Card with number 19450920-14121-00001-15. As in lieu thereof do assume and adopt the name of ERNESTER BARTHOLOME KIMARIO.
And in pursuance of such change of name as aforesaid I hereby declare that I shall at all times hereafter in all records, deeds and instruments in writing and in all actions and proceedings and in all dealings and transactions and upon all occasions whatsoever related to my professional, use and sign the name of ERNESTER BARTHOLOME KIMARIO as my name in lieu of the said names of AMBROSIA BARTHOLOME KIMARYO renounced as aforesaid.
THAT the reason for such change is wrong registration of my names on my Public Pension Fund. Whereas my names read as ERNESTER BARTHOLOME KIMARIO.
AND I HEREBY AUTHORIZE and request all persons to designable and address me by such assumed name of ERNESTER BARTHOLOME KIMARIO.
IN WITNESS WHEREOF I have hereunder signed my assumed name of ERNESTER BARTHOLOME KIMARIO, and have set my hand this 16th day of January, 2023.

SIGNED and DELIVERED
AMBROSIA BARTHOLOME KIMARYO
ERNESTER BARTHOLOME KIMARIO
BEFORE ME
COMMISSIONER FOR OATHS
DRAWN BY:
ZAINAB S NTARAMBE
ADVOCATE
DEPONENT



Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

## Rais Zambia: Acheni mambo ya kuchunguzana

**LUSAKA,** Zambia

RAIS wa Zambia, Hakainde Hichilema (pichani), amewataka raia wa nchi hiyo kuacha kuchunguza simu za wenzi wao, ikiwa ni sehemu ya maoni yake yanayolenga kupunguza viwango vya talaka katika taifa hilo.

Rekodi zinaonyesha kuwa nchi hiyo ilirekodi zaidi ya kesi 22,000 za talaka mwaka jana pekee, takwimu ambazo rais alizitaja kuwa za kusikitisha.



Ilibainishwa kuwa jana, ukosefu wa haki za ndoa, uzinzi, unyanyasaji wa kijinsia, matusi na ukatili ni miongoni mwa sababu kuu za watu waliotajwa katika mahakama za kutaka talaka.

"Tunaoana kwa ajili ya mapenzi, hatuoi ili kwenda kuangaliana au kwenda kunyoosheana kidole, uhuru unamaanisha uwajibikaji katika kuweka mipaka uhuru wetu, si kuchezea uhuru wa wengine, kuwa mvumilivu, uwe mwenye kuelewa," alisema Hichilema.

Hata hivyo takwimu za miezi 12 iliyopita zilionyesha ndoa fupi zaidi nchini humo ilidumu kwa siku 30 huku ndefu zaidi ikiwa ni miaka 65. **BBC**

## Russia kujiunga kwenye mazoezi na Afrika Kusini

**MOSCOW,** Russia

SHIRIKA la habari la serikali la Russia la Tass linaripoti likinukuu chanzo cha kijeshi kuwa meli ya kivita ya Russia iliyobeba silaha itashiriki katika mazoezi ya pamoja na wanajeshi wa majini wa China na Afrika Kusini mwezi Februari.

Shirika la habari la Reuters lilibainisha jana kuwa ni mara ya kwanza kutajwa rasmi kwa ushiriki wa meli hiyo ya kivita, ambayo ina silaha za makombora ya Zircon.

"Meli hiyo itakuwa katika kituo cha usafirishaji katika bandari ya Syria ya Tartus na baada ya hapo itashiriki katika mazoezi ya pamoja na wanamaji wa China na Afrika Kusini," Tass ilisema.

Siku ya Alhamisi Jeshi la Afrika Kusini lilitangaza mwezi ujao kuwa litafanya mazoezi ya pamoja ya kijeshi na Russia na China katika pwani yake.

Mazoezi hayo yatafanyika kwa siku 10 kuanzia Februari 17 hadi 27, mwaka huu katika mji wa Bandari wa Durban na Richards Bay.

Jeshi la Ulinzi la Kitaifa la Afrika Kusini lilisema kuwa lengo la mazoezi hayo ni kubadilishana ujuzi na maarifa ya kiutendaji. **BBC**

# EU kujadili msaada zaidi dhidi ya Ukraine

**BRUSSELS,** EU

MAWAZIRI wa Mambo ya Nje wa Umoja wa Ulaya (EU) wanakutana Brussels kujadili suala la kuipatia msaada wa ziada Ukraine, lakini wanatarajiwa kujadili kuhusu Iran na kutangaza majina 37 kwenye orodha ya Wairan watakaowekewa vikwazo kutokana na ukiukwaji wa haki za binadamu.

Mkuu wa sera za nje wa EU, Josep Borrell, akiwa katika mkutano wa mawaziri wa mambo ya nje wa umoja huo jana, alisema anataraji nchi 27 wanachama zitaidhinisha fungu jingine la euro milioni 500 zaidi ya Sh. bilioni 127 za msaada wa kijeshi kwa ajili ya Ukraine.

Fedha hizo kwa mujibu wa Borrell ni sehemu ya kile kinachoitwa hazina ya amani ya EU ambayo ni bajeti ya ziada ya kuuwezesha umoja huo kuwa tayari kusimamia usalama duniani.

Wiki iliyopita zilikuwapo ripoti zilizoonyesha kwamba Hungary iliipinga hatua hiyo ingawa jana waziri wa mambo ya nje na msemaji wa serikali ya mjini Budapest alikataa kutoa tamko lolote kuhusu ripoti hizo.

**chi za EU pia zinashughulikia suala la vikwazo kadhaa vinavyotarajiwa kuanza kutekelezwa mwezi ujao dhidi ya Russia kutokana na uvamizi wake wa kijeshi nchini Ukraine.**

Aidha, Waziri wa Mambo ya Nje wa Ujerumani, Annalena Baebock, alisema Ujerumani haiwezi kuizuia Poland ikiwa nchi hiyo inataka kupeleka vifaru vya kivita chapa Leopard nambari 2 nchini Ukraine.

Waziri Mkuu wa Poland, Mateusz Morawiecki, alisema nchi yake itaiomba ridhaa Ujerumani kuhusu kupeleka vifaru hivyo vya kivita na kwamba mtazamo uliotolewa na Ujerumani unaonyesha kuna uwezekano wa kupatikana mwafaka juu ya suala hilo.

Nchi za EU pia zinashughulikia suala la vikwazo kadhaa vinavyotarajiwa kuanza kutekelezwa mwezi ujao dhidi ya Russia kutokana na uvamizi wake wa kijeshi nchini Ukraine.

Hayo yalielezwa na vyanzo vya kidiplomasia ingawa inatajwa kwamba hakuna maamuzi yanayotarajiwa kutolewa kwenye mkutano wa jana.

Hata hivyo, mawaziri wa mambo ya nje walijadili kuhusu kutumia mali ya Russia iliyozuiwa katika nchi za EU ambazo ziko chini ya vikwazo zikijumuisha akiba ya fedha euro bilioni 300 zaidi ya Sh. trilioni 762 ambazo zitatumiwa kusaidia kuijenga upya Ukraine.

Mkuu wa sera za nje wa EU Borrell, alisema hawawezi kuliorodhesha jeshi la ulinzi wa mapinduzi ya Iran katika orodha ya magaidi hadi pale mahakama ya umoja huo itakapotoa uamuzi wa kusema ni magaidi.

Vile vile mawaziri wanaokutana Brussels wameshajiandaa kuyaongeza majina 37 ya Wairan na taasisi za nchi hiyo katika orodha ya EU ya vikwazo kutokana na ukiukwaji wa haki za binadamu unaofanyika katika Jamhuri hiyo ya kiislamu.

Bunge la Umoja huo wiki iliyopita lilitoa wito wa jeshi la kimapinduzi la Iran litiwe kwenye orodha ya magaidi kutokana na ukandamizaji dhidi ya waandamanaji wa Iran pamoja na hatua yake ya kuipelekea Russia droni. **DW**



Mfalme wa Eswatini, Mswati wa tatu akihutubia mkutano wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa, Septemba 25, 2019. **PICHA: AP**

# Mwanasiasa mpinzani auawa Eswatini

**MBABANE,** Eswatini

WATU wenye silaha nchini Eswatini wamemuua mwanasiasa mashuhuri wa upinzani na mwanasheria wa haki za binadamu Thulani Maseko nyumbani kwake, saa chache baada ya mfalme wa nchi hiyo kuwashutumu wanaharakati wanaopinga utawala wake.

Hayo yalibainishwa jana na msemaji wa chama chake Sikelela Dlamini, akieleza kuwa Maseko aliuawa kwa kupigwa risasi Jumamosi usiku na washambuliaji wasiojulikana huko Luhleko, umbali wa kilomita 50 na mji mkuu Mbabane.

Msemaji huyo alisema aliambiwa wauaji walimpiga risasi kupitia dirisha akiwa ndani ya nyumba na familia yake.

Serikali ilituma salamu za rambirambi kwa familia yake, ikisema kifo cha Maseko ni hasara kwa taifa na kwamba polisi wamekuwa wakiwasaka walioamua.

Maseko alikuwa mwanasheria kiongozi wa haki za binadamu na mwandishi wa maoni nchini Eswatin, ambaye alikuwa na kesi inayoendelea mahakamani dhidi ya uamuzi wa Mfalme Mswati wa tatu kubadili jina la nchi na kuipa jina la Eswatini kwa amri.

Jina la nchi lilibadilishwa kutoka Swaziland na kuitwa Eswatini kwa kuadhimisha miaka 50 ya uhuru wake kutoka kwa Uingereza mwaka 2018.

Msimamo wa Maseko ulikuwa kwamba Mfalme hakufuata utaratibu wa katiba. **VOA**

HABARI MICHEZO

# DSTV, UNGCT KUPANDA MAMILIONI YA MITI NCHINI

Na Mwandishi Wetu

DSTV Tanzania kwa kushirikiana na wakala wa Umoja wa Mataifa (UN Global Compact) wamezindua mradi wa kuhifadhi na kuboresha mazingira unaojulikana kama BeGreen wenye lengo la kupanda miti katika maeneo ya umma ikiwa ni mkakati wa kuhifadhi mazingira.

**Kwa kuanzia mradi huo umetoa miti 2,000 kwa shule 10 za Halmashauri ya Chalinze ambazo ni Bwilingu A, Bwilingu B, Kibiki, Msoga, Chalinze, Chahua, Beracha Valley, Moreto, Msata na Chalinze Islamic.**

Akizunguza wakati wa hafla ya kukabidhi miche ya miti hiyo kwa shule husika, Mbunge wa Chalinze na Naibu Waziri wa Ardhi, Ridhiwani Kikwete alisema mradi huo umekuja wakati muafaka kwani suala la uharibifu wa mazingira limekuwa sugu na lenye athari mbaya kwa jamii.

Alisema mradi huo utasaidia sana kuboresha mazingira kwani unatoa miti ya aina mbalimbali ikiwamo ya matunda, kivuli na hata ya mbao.

"Tunawashukuru sana wadau wetu wa DStv na UN Global Compact Tanzania kwa kuja na mradi huu muhimu. Kwetu sisi wana Chalinze tunaupokea kwa mikono miwili kwani tumekuwa na mipango ya kuhifadhi na kuboresha mazingira yetu na suala la upandaji miti na uhifadhi wa misitu na uoto wa asili kwa ujumla ni suala tunalolipa uzito mkubwa," alisema Kikwete.

Aidha aliwataka walimu na wanafunzi wa shule hizo kuhakikisha kuwa miti hiyo inatunzwa na kustawi na pia kuendelea kupanda miti katika maeneo yao.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa UN Global Compact Tanzania, Marsha Yambi, alisema kuhifadhi mazingira ni moja ya vipaumbele vyao na wanafurahi kuona kuwa wamepata mdau kama DStv katika kufanikisha mradi huu.

Alimshukuru Mbunge wa Chalinze kwa kutoa ushirikiano mkubwa uliowezesha zoezi hili kufanikiwa na kuahidi kuwa huo ni mwanzo na wataendelea kupanda miti katika maeneo mbalimbali ya umma ili kuhifadhi na kuboresha mazingira.

Naye Mkuu wa Uhusiano wa DStv Tanzania, Johnson Mshana, alisema kuwa mradi huo ni sehemu ya ushiriki wa DStv katika miradi mbalimbali inayoigusa jamii moja kwa moja.

Hafla hiyo ya kukabidhi miti 2,000 kwa shule za Chalinze ilifanyika katika Shule ya Msingi Bwilingu A na kuhudhuriwa na walimu kutoka shule husika, viongozi wa Halmashauri ya Chalinze, Diwani wa Kata ya Bwilingu na wanafunzi wa shule husika.



Naibu Waziri wa Ardhi na Mbunge wa Chalinze, Ridhiwani Kikwete (katikati), akiwa na Mkurugenzi wa UN Global Compact Network Tanzania, Marsha Yambi (kushoto), na Mkuu wa Uhusiano wa DStv Tanzania, Johnson Mshana (kulia), wakipanda mti katika Shule ya Msingi Bwilingu A kuashiria kuzinduliwa kwa mradi wa BeGreen unaendeshwa na wakala wa Umoja wa Mataifa (UNGCNT) kwa kushirikiana na DStv Tanzania. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Kidunda: Nakuja kivingine mwaka 2023

Na Saada Akida

KUELEKEA pambano la kuwania mkanda wa ubingwa wa Afrika Boxing Union (ABU) katika uzito wa Super Middle, bondia wa ngumi za kulipwa nchini, Selemani Kidunda amesema mwaka 2023 anakuja kivingine hasa kwa mchezo wake huo utakaopigwa Februari 24.

Kidunda atapanda ulingoni dhidi ya Patrick Mukala kutoka Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), na litasindikiwa na pambano la kisasi kati ya Oscar Richard dhidi ya Adam Mbega, litafanyika katika ukumbi wa Ubungo Plaza jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kidunda alisema anaendelea kufanya mazoezi ya kujiandaa vizuri kwa mwaka huu 2023 nakuja kivingine tofauti na mwaka jana alivyopigana mjini Songea na Shimanga Katompa.

Alisema amekuja na mbinu mpya na staili mpya kwa sababu ya mpinzani wake kumfuatilia mapambano yake ya nyuma aliyowahi kucheza ikiwamo ya mwaka jana.

"Nafurahi kupata nafasi hii ya kupanda ulingoni mwaka 2023, itakuwa mechi yangu ya kwanza naendelea na maandalizi mazuri na nakuja kivingine kabisa na Watanzania wataona ngumu bora kabisa Februari 24," alisema Kidunda.

Kwa upande wa promota wa pambano hilo kutoka Kampuni ya Kemmon Sports Agency, Saadah Salum, alisema lengo la kuandaa pambano hilo ni kuhakikisha wanaendelea kukuza na kutangaza mchezo wa ngumi kwa Tanzania.

Alisema pambano hilo litakuwa la ushindani mkubwa kwa sababu ya mabondia hao kuwa na rekodi nzuri katika mapambano yaliyopita.



# Kibo Palace kuendelea kudhamini Kilimanjaro Marathon

Na Mwandishi Wetu

UONGOZI wa Kibo Palace Hotels umesema utaendelea kudhamini mbio za kila mwaka za Kilimanjaro Premium Lager International Marathon kutokana na umuhimu wake katika kukuza uchumi wa taifa, vipaji vya michezo na michezo kwa ujumla hapa nchini.

Ahadi hiyo ilitolewa na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa kampuni inayomiliki hoteli za Kibo Palace, Vincent Laswai, wakati wa hafla ya uzinduzi wa mbio hizo toleo la Mkoa wa Kilimanjaro iliyofanyika hotelini hapo, Moshi, mkoani Kilimanjaro hivi karibuni.

"Mbio za kimataifa za Kilimanjaro Premium Lager International Marathon zimetoa na zinaendelea kutoa mchango mkubwa katika kukuza michezo, hasa kuibua na baadaye kukuza vipaji vipya katika riadha, pamoja na kuinua uchumi hasa katika sekta ya utalii," alisema.

Aliongeza, "Sisi katika sekta ya utalii ndio mashahidi wakuu wa maboresho haya katika sekta ya utalii na hii ni kwa sababu tunawapokea na kuwakaribisha wageni wengi wanaokuja kushiriki katika mbio hizi kila mwaka".

Alisema hoteli za Kibo Palace zinajivunia kuhusishwa na michuano hii ya kila mwaka inayotambulika duniani kwa sasa ambayo alisema ina mchango mkubwa katika kuitangaza Tanzania nje ya nchi na hivyo kuongeza idadi ya watalii wanaotembelea Mkoa wa Kilimanjaro na nchi nzima kwa ujumla.

Kwa Arusha Kibo Palace inaendesha Kibo Palace Hotel na kwa Moshi ni Kibo Palace Homes na Kibo Palace Hotel.

Mbio za 21 za Kilimanjaro Premium Lager International Marathon zinatarajiwa kufanyika Februari 26, mwaka huu, katika viwanja vya Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU), ambapo zinatarajiwa kuhusisha zaidi ya washiriki 12,000 kutoka zaidi ya nchi 50 duniani.

Mashindano hayo ambayo yanayoandaliwa na Kilimanjaro Marathon Company Limited na kuratibiwa kitaifa na Kampuni ya Executive Solutions Limited, yamedhaminiwa na Kilimanjaro Premium Lager ambao ndiyo wadhamini wakuu kupitia udhamini wao wa mbio za kilomita 42 na Tigo ambao ni wadhamini wa mbio za Tigo Half-Marathon za kilomita 21.

Wadhamini wengine mbali na kampuni ya hoteli za Kibo Palace, ni pamoja na Simba Cement, Kilimanjaro Water, TPC Sugar, Total Energies, wasambazaji rasmi GardaWorld Security, Keys Hotel na CMC Automobiles.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### RICE KUTUA ARSENAL

KIUNGO wa kati wa West Ham, Declan Rice, 24, anaelekea kujiunga na Arsenal msimu wa joto, huku Chelsea na Manchester United pia zikitarajiwa kuwania saini ya mchezaji huyo wa kimataifa wa England. ***(Guardian)***

### LAMPARD HALI TETE

MMILIKI wa Everton, Farhad Moshiri amefanya mazungumzo na bodi ya klabu hiyo kuhusu mustakabali wa kocha Frank Lampard na mtu mwenye uwezekano wa kuchukua nafasi ya kiungo huyo wa zamani wa England, iwapo atatimuliwa. ***(Telegraph)***

### CONTE HATAKI

MKATABA wa Kocha wa Tottenham Hotspur, Antonio Conte, 53, unamalizika msimu huu wa joto na akiwa tayari amepewa mkataba mpya, kocha huyo amewataka Spurs kuuweka kando mkataba huo kwa sababu hataki kufikiria mustakabali wake kwa sasa. ***(Sky Sports)***

### TROSSARD ALITAKIWA SPURS

WAKALA wa mshambuliaji wa Ubelgiji, Leandro Trossard, 28, amesema Tottenham Hotspur walikuwa kwenye mazungumzo ya kumsajili mchezaji huyo kabla ya kujiunga na wapinzani wa London kaskazini Arsenal, ambao walikuwa na maamuzi madhubuti kufanikisha uhamisho huo. ***(Mirror)***

### GIL AWEKWA CHAMBO SPURS

WINGA wa Hispania, Bryan Gil, 21, anaaminika kuwa mmoja wa wachezaji watatu ambao Tottenham Hotspur inawapa AS Roma kama sehemu ya mpango wa kubadilishana na kiungo wa Italia, Nicolo Zaniolo, 23. ***(Football Insider)***

### ZANIOLO HAONDOKI

KOCHA wa AS Roma, Jose Mourinho anafikiri Nicolo Zaniolo huenda asiondoke kwa sababu ofa zilizofika mezaji kwa ajili ya mchezaji huyo "hazifai kwake wala klabu". ***(Football Italia)***

### ZIYECH AWINDWA ROMA

AS Roma imefanya mawasiliano ya awali na wakala wa winga wa Chelsea, Hakim Ziyech, 29, na wanaweza kumnunua winga huyo wa Morocco ikiwa watamuuza Nicolo Zaniolo. ***(Sky Sports Italia)***

### EVERTON YAMNYATIA HAKIM

KLABU ya Everton pia inataka kumleta Hakim Ziyech kusaidia vita vyao vya kuepuka kushuka daraja na wangependelea kumsajili kwa mkopo kwa nia ya kufanya uhamisho huo kuwa wa kudumu iwapo wataepuka kushuka. ***(Mail)***

### ROQUE AWANIWA MAN

KLABU ya Manchester United imejiunga na Paris St-Germain katika kumsaka Mbrazil, Vitor Roque, 17, ambaye ana kipengele cha kuuzwa kwa pauni milioni 52.5 katika mkataba wake wa Athletico Paranaense. ***(Gazzetta dello Sport)***

### NAVAS AGOMBEWA

KLABU ya Nottingham Forest inatazamia kumsajili kipa wa PSG, Keylor Navas, 36, huku Dean Henderson, 25, akikabiliwa na majeraha ya muda mrefu, ingawa Bournemouth na Leicester City pia zinavutiwa na mchezaji huyo wa Costa Rica. ***(Mundo Deportivo)***

## DONDOO KA
## MAGAZET A




# ARTETA: NKETIAH ANA ROHO HALISI YA ARSENAL

**LONDON,** England

Asifia kiwango chake, asema hakufikiria kama angeweza kuwa bora...

MIKEL Arteta hakufikiria kabisa kwamba, Eddie Nketiah angeweza kucheza kwa kiwango bora msimu huu na amemsifia mchezaji huyo kuwa ana "moyo na roho halisi ya Arsenal".

**Nketiah sasa ndiye mfungaji bora wa Arsenal msimu huu akiwa amefunga mabao tisa katika michuano yote na alifunga mara mbili katika ushindi wa 3-2 dhidi ya Manchester United, Jumapili.**

Ana mabao manne kwenye Ligi Kuu ya England licha ya kuanza mechi tano pekee - wastani wa bao kila baada ya dakika 147 baada ya kuanza msimu kama msaidizi wa Gabriel Jesus, ambaye aliumia kwenye Kombe la Dunia.

Arteta alikuwa na imani na Nketiah kuongeza hatua lakini alikubali kwamba kulikuwa na ushahidi mdogo wa kiwango cha "ajabu" ambacho mshambuliaji huyo anacheza sasa.

"Anachofanya Eddie ni cha kushangaza," alisema Arteta. "Hatuwezi kusema tuliona kwamba anakuja, tulitarajia angeweza kufanya hivyo, kwa sababu ya jinsi alivyo, kwa sababu ya mawazo yake, kwa sababu ya sifa zake na jinsi sifa hizo zinafaa ndani ya timu.

"Kumpoteza Gabby lilikuwa pigo kubwa, lakini majibu ya Eddie ametoa kwa njia ya kipekee."

Alipoulizwa ni nini alichoona kwa Nketiah, Arteta alijibu: "Sifa alizonazo, anataka kiasi gani, ana imani kiasi gani kwake kuwa namba tisa wa Arsenal ndio nia yake.

"Tuko naye kila siku. Yeye ni mtoto maalum, anayependwa sana na kila mtu. Ana moyo na roho ya kweli ya Arsenal ndani yake. Huwezi kuweka hilo katika namba, lakini yeye ni mzuri sana."

Nketiah alipiga mashuti sita dhidi ya Man United na ilionekana kana kwamba angepoteza nafasi hiyo ya kupata ushindi mnono aliponyimwa na David de Gea bao dakika sita kabla ya bao lake la dakika za mwisho na la ushindi.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,069,8

JACKPOT MECHI WIKI HII

TAREHE: 25,26 NA 27 JANUARI 2023

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 25/01/23 | 20:30 | Mainz vs Borussia Dortmund | 2.83 | 3.52 | 2.26 |
| 02. 25/01/23 | 22:00 | Fortuna Sittard vs Heerenveen | 2.82 | 3.36 | 2.34 |
| 03. 25/01/23 | 22:30 | SC Freiburg vs Eintracht Frankfurt | 2.46 | 3.42 | 2.63 |
| 04. 25/01/23 | 22:30 | Augsburg vs Monchengladbach | 2.96 | 3.40 | 2.23 |
| 05. 25/01/23 | 22:30 | Werder Bremen vs Union Berlin | 2.73 | 3.13 | 2.53 |
| 06. 26/01/23 | 00:00 | Osasuna vs Sevilla FC | 2.32 | 3.08 | 3.13 |
| 07. 26/01/23 | 02:30 | Santo Andre SP vs Botafogo SP | 2.63 | 2.94 | 2.63 |
| 08. 26/01/23 | 10:45 | Melbourne Victory vs Sydney FC | 2.51 | 3.25 | 2.71 |
| 09. 26/01/23 | 14:00 | Aizawl FC vs Mohammedan SC | 2.81 | 3.22 | 2.31 |
| 10. 26/01/23 | 20:45 | Groningen vs Cambuur | 2.19 | 3.37 | 3.07 |
| 11. 26/01/23 | 22:00 | Valencia vs Athletic Bilbao | 2.70 | 3.08 | 2.63 |
| 12. 27/01/23 | 06:00 | Club Atlas vs Santos Laguna | 2.66 | 3.30 | 2.53 |
| 13. 27/01/23 | 11:45 | Newcastle Jets vs Brisbane Roar | 2.76 | 3.23 | 2.48 |

KUWEKA PESA:

- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.

tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money

SEND

SportPesa

SPORTPESA.CO.TZ

PIGA *150*87#

GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# TEN HAG ATAKA WACHEZAJI MAN UNITED KUBADILIKA



**LONDON,** England

ERIK ten Hag aliona kufungwa kwa Manchester United dhidi ya Arsenal kama ushahidi kwamba lazima "kubadilisha mawazo yetu" ili kushindana "kwenye kiwango cha juu".

United walikubali bao la dakika za lala salama kwa mara ya pili wiki hii, wakianza kwa bao la kusawazisha la Michael Olise kwa Crystal Palace likifuatiwa na la ushindi la Eddie Nketiah kwenye Uwanja wa Emirates, Jumapili.


Bao la Nketiah dakika ya 90 liliipa Arsenal ushindi wa 3-2 waliostahili zaidi.

Kocha huyo wa Man United bado alihisi wangeweza na walipaswa kuondoka na pointi. Alirejelea ujumbe aliokuwa amewapa wachezaji wake, akiwaambia nyota wake wa United bado hawajawa tayari kushinda mataji makubwa.

"Labda katika saa chache zijazo, nitagundua tuko katika nafasi nzuri, tambua tuko katika maendeleo mazuri, mchakato mzuri," alisema Ten Hag. "Lakini kwa wakati huu, nina hasira.

"Pia niliwaambia wachezaji: 'Ikiwa unataka kushinda mataji, lazima tubadilishe mawazo yetu.' "Haiwezekani katika mchezo wa juu unafanya makosa matatu makubwa kiasi kwamba unaruhusu mabao.

"Hasa bao la mwisho, hivyo lazima uchukue hatua. Huwezi kutoa bao kama hilo, kama tulivyofanya, kwenye kiwango cha juu. Basi huwezi kushinda mataji.



## *Di Maria atoa msimamo wake Juve*

**TURIN,** Italia

ANGEL Di Maria amesisitiza kukatwa kwa pointi za Juventus hakutaathiri mustakabali wake mjini Turin huku akiwataka Bianconeri hao kupigania kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Bao la Danilo la dakika ya 65 liliokoa na kuwapa Juve sare 3-3 dhidi ya Atalanta Jumapili, siku mbili tu baada ya Juve kupokonywa pointi 15 kufuatia uchunguzi wa shughuli zao za awali za uhamisho.

Juve wameripotiwa kukata rufaa dhidi ya adhabu hiyo, lakini kikosi hicho cha kocha Massimiliano Allegri kinakabiliwa na kibarua kigumu kumaliza katika nafasi nne za juu kwenye Ligi Kuu ya Italia, Serie A, wakiwa nyuma ya AS Roma walio nafasi ya nne kwa pointi 14.

Di Maria anatumaini vijana wa Allegri, ambao walikuwa wa tatu kabla ya uamuzi wa Ijumaa, wanaweza kufukuzia katika timu nne bora za Italia na nafasi ya kushiriki Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao huku akielezea kujitolea kwake kwa Bianconeri.

"Ni vigumu kuwa juu kwa pointi 20, lakini ikiwa tutaendelea kufanya kazi na mawazo haya tunaweza kufanya kitu cha ajabu," alisema Di Maria, ambaye alisaini mkataba wa mwaka mmoja Julai, akiiambia DAZN.

"Hakuna kinachoshindikana hapa.

## HABARI MICHEZO

# 361,169/-

## SUPA JACKPOT MECHI WIKI HII

### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 28/01/23 | 18:00 | Hull City vs Queens Park Rangers | 2.50 | 3.30 | 2.70 |
| 02. 28/01/23 | 18:00 | Blackburn Rovers vs Birmingham City | 2.27 | 3.20 | 3.15 |
| 03. 28/01/23 | 23:00 | Getafe CF vs Real Betis Seville | 2.95 | 2.95 | 2.55 |
| 04. 29/01/23 | 14:15 | FC Twente Enschede vs Feyenoord Rotterdam | 2.75 | 3.45 | 2.40 |
| 05. 29/01/23 | 15:00 | OGC Nice vs Lille OSC | 2.95 | 3.30 | 2.35 |
| 06. 29/01/23 | 15:30 | RSC Anderlecht vs Royal Antwerp FC | 2.75 | 3.25 | 2.50 |
| 07. 29/01/23 | 16:00 | Real Valladolid vs Valencia CF | 3.10 | 3.25 | 2.28 |
| 08. 29/01/23 | 16:30 | Brighton & Hove Albion vs Liverpool FC | 2.65 | 3.50 | 2.45 |
| 09. 29/01/23 | 17:00 | AJ Auxerre vs Montpellier HSC | 2.45 | 3.30 | 2.80 |
| 10. 29/01/23 | 17:00 | Clermont Foot 63 vs FC Nantes | 2.37 | 3.30 | 2.90 |
| 11. 29/01/23 | 17:30 | Schalke 04 vs 1. FC Cologne | 2.95 | 3.40 | 2.29 |
| 12. 29/01/23 | 18:00 | Cercle Brugge vs KAA Gent | 3.05 | 3.30 | 2.29 |
| 13. 29/01/23 | 18:15 | CA Osasuna vs Atletico Madrid | 3.20 | 3.20 | 2.26 |
| 14. 29/01/23 | 18:45 | SC Cambuur vs Fortuna Sittard | 2.75 | 3.35 | 2.45 |
| 15. 29/01/23 | 19:30 | Bayer Leverkusen vs Borussia Dortmund | 2.46 | 3.50 | 2.65 |
| 16. 29/01/23 | 20:30 | RC Celta de Vigo vs Athletic Bilbao | 2.85 | 3.00 | 2.55 |
| 17. 29/01/23 | 21:00 | Boavista Porto vs Portimonense SC | 2.27 | 3.20 | 3.15 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMANNE - 24/01/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 3796 | Churchill Brothers vs Real Kashmir | 1.96 | 3.27 | 3.53 |
| 15:45 | 5474 | Coca Cola vs Al Masry Club | 2.28 | 2.87 | 3.47 |
| 16:00 | 1193 | KMC vs Namungo | 2.13 | 2.70 | 3.30 |
| 16:30 | 3372 | AL Wakrah vs Al-Sailiya SC | 1.51 | 4.09 | 5.17 |
| 16:30 | 3768 | Qatar SC vs Umm-Salal SC | 2.20 | 3.21 | 3.00 |
| 18:00 | 2489 | Ahli AL Khalil vs Shabab Al Dhahiriya | 3.55 | 3.30 | 1.81 |
| 18:00 | 2493 | Ghazl EL Mahallah vs Zamalek | 4.68 | 3.48 | 1.74 |
| 19:00 | 1891 | Mauritania vs Mali | 3.60 | 3.05 | 2.16 |
| 19:00 | 3396 | Al Gharafa SC vs Al Rayyan SC | 2.04 | 3.53 | 3.06 |
| 20:00 | 2496 | Smouha Club vs Pyramids | 6.16 | 3.63 | 1.57 |
| 20:00 | 3027 | Al Ahly Cairo vs National Bank | 1.37 | 4.57 | 7.94 |
| 20:30 | 4005 | TS Galaxy FC vs Mamelodi Sundowns | 3.53 | 3.22 | 2.06 |
| 20:30 | 4084 | Schalke 04 vs RB Leipzig | 5.14 | 4.15 | 1.55 |
| 20:45 | 2952 | Emmen vs PSV Eindhoven | 6.74 | 4.75 | 1.39 |
| 21:00 | 3063 | Borussia Dortmund II vs Osnabruck | 3.12 | 3.59 | 2.08 |
| 22:00 | 3488 | Niger vs Cameroon | 3.75 | 2.95 | 2.16 |
| 22:00 | 4196 | Telstar vs Maastricht | 1.90 | 3.52 | 3.63 |
| 22:30 | 3712 | Hoffenheim vs Stuttgart | 1.99 | 3.56 | 3.37 |
| 22:30 | 4953 | Hertha BSC vs VfL Wolfsburg | 2.77 | 3.32 | 2.40 |
| 22:30 | 5992 | Bayern Munchen vs FC Koln | 1.18 | 7.13 | 10.90 |
| 22:45 | 1283 | Larne vs Portadown FC | 1.12 | 7.05 | 15.54 |
| 22:45 | 1394 | Glentoran Belfast vs Dungannon Swifts | 1.20 | 5.38 | 12.41 |
| 22:45 | 1598 | Bolton vs Forest Green | 1.45 | 4.27 | 6.36 |
| 22:45 | 1736 | Port Vale vs Derby | 3.27 | 3.27 | 2.14 |
| 22:45 | 2360 | Crawley Town vs Grimsby | 3.27 | 3.27 | 2.13 |
| 22:45 | 2995 | Maidstone vs Aldershot | 2.48 | 3.31 | 2.63 |
| 22:45 | 3048 | Wycombe vs Oxford Utd | 2.24 | 3.37 | 2.97 |
| 22:45 | 3081 | Carlisle vs Hartlepool | 1.55 | 3.81 | 5.74 |
| 22:45 | 3265 | Lazio vs AC Milan | 2.96 | 3.30 | 2.28 |
| 22:45 | 3521 | Swindon Town vs Stevenage | 3.02 | 3.16 | 2.31 |
| 22:45 | 3771 | Burton vs Peterborough | 2.92 | 3.42 | 2.25 |
| 22:45 | 3928 | Dundee FC vs Dunfermline | 1.78 | 3.42 | 4.04 |
| 22:45 | 4019 | MK Dons vs Shrewsbury | 2.20 | 3.22 | 3.17 |
| 22:45 | 4450 | Cheltenham vs Sheffield Wed | 4.76 | 3.77 | 1.66 |
| 22:45 | 4881 | Linlithgow Rose FC vs Raith Rovers | 5.19 | 4.10 | 1.51 |
| 22:45 | 4989 | FC Arouca vs Sporting Lisbon | 6.64 | 4.46 | 1.38 |
| 22:45 | 5033 | Fleetwood Town vs Portsmouth | 2.93 | 3.18 | 2.36 |
| 22:45 | 5261 | Exeter vs Barnsley | 2.66 | 3.26 | 2.52 |
| 22:45 | 5396 | Crusaders Belfast vs Linfield Belfast | 2.58 | 3.31 | 2.44 |
| 22:45 | 5452 | Colchester vs Salford City | 2.82 | 3.17 | 2.44 |
| 22:45 | 5640 | Accrington vs Boreham Wood | 2.15 | 3.25 | 3.20 |
| 22:45 | 5772 | Ballymena Utd vs Newry City AFC | 1.87 | 3.54 | 3.54 |
| 22:45 | 5819 | AFC Wimbledon vs Walsall | 2.40 | 3.12 | 2.92 |
| 22:45 | 5842 | Ipswich vs Morecambe | 1.25 | 5.56 | 9.93 |
| 22:45 | 5880 | Stockport vs Bradford City | 1.75 | 3.58 | 4.37 |
| 22:45 | 5940 | Elgin City vs Drumchapel United | 1.28 | 5.20 | 7.91 |
| 22:45 | 5960 | Coleraine FC vs Carrick Rangers | 1.35 | 4.66 | 7.04 |
| 22:45 | 5989 | Glenavon vs Cliftonville Belfast | 3.26 | 3.47 | 1.98 |
| 23:00 | 1735 | Southampton vs Newcastle | 4.47 | 3.53 | 1.76 |
| 23:00 | 4755 | Sparta Rotterdam vs Waalwick | 1.84 | 3.40 | 4.14 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# MWIJAKU ATABIRI KIFO CHA BONGO FLEVA, TAARAB

**Na Sabato Kasika**

MSANII wa maigizo Burton Mwambe 'Mwijaku' amesema baada ya miezi sita ijayo kuanzia sasa, muziki wa kizazi kipya (bongo fleva) na taarab utafutika na kwamba dansi itarudi kwenye kilele kama ilivyokuwa miaka ya nyuma.

**Mwijaku ametaja sababu ya kutabiria kifo bongo fleva na taarab kuwa ni wasanii kukosa ubunifu, kitendo kinachosababisha mashabi-ki kuuchoka na kuamua kurudi kwenye dansi.**

Nyota huyo ambaye ni msemaji wa bendi ya Town Classic, alitoa utabiri huo wakati akizungumzia bonanza la bendi hiyo linalotarajiwa kuanza Jumapili ijayo, katika ukumbi wa Msasani Beach, jijini Dar es Salaam.

"Hakuna ubishi kwamba, muziki wa bongofleva na taarabu utakufa baada ya miezi ijayo, wasanii wake hawana ubunifu, dansi itakuwa juu, kwa sababu mbinu zote za kupandisha dansi tunazijua," alisema Mwijaku.

Mwijaku alisema bendi ya kwanza kuwa juu baada ya miezi sita ni Town Classic, kwa madai kwamba, inaundwa na wanamuziki wabunifu, wachapakazi na wenye vipaji vya hali ya juu.

"Wale ambao hawaamini ninachosema, waje katika bonanza litakaloanza Januari 29 waone kile ambacho vijana wa Town Classic Band wanakifanya kwa ajili ya kurudisha hadhi ya muziki wa dansi," alisema.

Alisema hiyo ndio ahadi yake kwamba wanakwenda kuzika bongofleva na taarab na kurejesha muziki wa dansi kupitia Town Classic Band, ili mashabiki wapate uhondo ambao waliukosa kwa muda mrefu.

Msemaji huyo alifafanua kuwa bendi hiyo imedhamiria kurejesha hadhi ya muziki wa dansi na si kuharibu bendi nyingine na kwamba mashabiki ndio watakaoamua ni wapi waende kupata burudani ya uhakika.



Msemaji wa bendi ya Town Classic, Burton Mwambe 'Mwijaku' (katikati), akizungumzia utabiri wake kuhusu bongofleva na taarab. Kulia ni meneja wa bendi hiyo, Andrew Sekidia na rapa Totoo Kalala. **PICHA: SABATO KASIKA**

## Mzize apambana kupata namba

INATOKA UKURASA 24

kupambana kujituma ili kujihakikisha nafasi ya kucheza kwenye kikosi cha timu kubwa.

"Ni kweli katika nafasi ninayocheza kuna watu wawili Mayele na Musonda, hao ni kaka zangu ninawaheshimu kwa sababu ni wakubwa kwangu, suala la kupata nafasi nina imani bado nitapata kwa sababu nitajituma na kufuata maelekezo ya benchi la ufundi ili kupata nafasi ya kucheza zaidi," alisema Mzize.

Alisema kazi kubwa iliyoko mbele yake ni kuhakikisha anapambana na kuonyesha uwezo mzuri, kuhakikisha Kocha Nesreddine Nabi kumwamini na kumpa nafasi ya kucheza kama ilivyo kwa michezo ya mzunguko wa kwanza tangu alipomtoa katika kikosi cha vijana.

## *Oliveira: Wachezaji Simba wamenielewa*

INATOKA UKURASA 24

poteza mechi ambayo walistahili kama si kushinda na kupata pointi tatu, basi hata kutoka sare na kuambulia pointi moja.

"Tumecheza vizuri sana mechi hii, tuliwasoma tunawatengenezea mfumo na wachezaji wanapambana sana, lakini Simba ni timu kubwa, walifunga bao kwa ukosefu wa mawasiliano kati ya beki na kipa wake. Kipindi cha pili tukarudi kwa nguvu, lakini hatukufanikiwa kupata bao, ndiyo mpira lakini tumepoteza mechi ambayo hatukustahili kutoambuliwa hata pointi moja," alisema Liogope.

Simba bado inaendelea kuhodhi nafasi ya pili ikifikisha pointi 50, huku Dodoma Jiji ikibakia na pointi zake 21 kwa mechi 21, kwenye nafasi ya 13 ya msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Michezo
Jumanne Januari 24, 2023
Nipashe



'Nketiah ana roho halisi ya Arsenal' UKURASA 21



Wachezaji wa Simba wakishangilia bao wakati wa mchezo wao dhidi ya Dodoma Jiji uliopigwa juzi kwenye Uwanja wa Jamhuri. **PICHA: SIMBA**

## Mzize sasa apambana kupata namba

**Na Saada Akida**

MSHAMBULIAJI kinda wa Yanga, Clement Mzize, amesema hatakata tamaa na ataendelea kujituma zaidi mazoezini ili kumshawishi kocha Nesreddine Nabi kumwamini na kuendelea kumpa nafasi.

Mzize amepandishwa kutoka kikosi cha timu ya vijana na sasa yuko kikosi cha timu kubwa akiungana na kinara wa mabao ndani ya kikosi hicho, Fiston Mayele na Kennedy Musonda aliyesajiliwa kwenye dirisha dogo.



Akizungumza na gazeti hili jana, Mzize alisema anatambua ushindani uliopo ndani ya timu hiyo katika safu ya ushambuliaji, anapambana na kujituma mazoezini na kufanya vizuri katika mechi kila anapopewa nafasi ili kuendelea kupata namba.

Alisema ni ngumu kupata nafasi ya kucheza mara kwa mara ndani ya kikosi cha kwanza hasa baada ya kuongezeka kwa mtu mwingine anacheza nafasi hiyo na

INAENDELEA UKURASA 23

# Oliveira: Wachezaji wamenielewa

**Na Adam Fungamwango**

## ●●● Akunwa na kiwango chao bila uwepo wa baadhi ya mastaa baada ya...

KOCHA Mkuu wa Simba, Roberto Oliveira, ameonesha kufurahishwa na ushindi wa bao 1-0 iliopata timu yake dhidi ya Dodoma Jiji juzi kwenye Uwanja wa Jamhuri Dodoma bila kuwapo kwa baadhi ya mastaa wake muhimu kwenye timu yake, huku akisema falsafa yake imeanza kuingia vichwani mwa wachezaji.

**Akizungumza baada ya mechi hiyo, kocha huyo ambaye ni mechi yake ya pili ya Ligi Kuu huku akishinda zote, aliwasifu wachezaji aliowapa nafasi kwa kucheza kwa maelekezo, akisema bado kidogo tu itakuwa tishio.**

Aliwasifu pia wachezaji wapya waliosajiliwa hivi karibuni ambao ni mechi yao ya kwanza kucheza, Jean Baleke aliyefunga bao pekee na Ismael Sawadogo akisema wameongeza kitu kwenye kikosi.

"Niwasifu wachezaji wangu, wamecheza vizuri leo (juzi) nimewapa nafasi wachezaji wengine ili waoneshe walichonacho kwa sababu hatukuwa na wachezaji wengi wa kikosi cha kwanza, na kweli wamepambana hadi tumepata ushindi, ninachoshukuru pia ni kuwa wameanza kuelewa falsafa yangu," alisema Oliveira.

"Simba ni timu kubwa, ushindi ilikuwa ni kitu kikubwa kwetu, tumepata nafasi mwishoni mwa kipindi cha kwanza tumeitumia na tulicheza vizuri, kipindi cha pili tuliamua kuubana uwanja ili kuzuia zaidi mashambulizi wa timu pinzani. Nimefurahishwa na wachezaji wapya ambao ni mara ya kwanza kucheza, wanaonekana watakuwa msaada sana baadaye, pia niwashukuru mashabiki kwa kujitokeza kwa wingi hapa uwanjani," aliongeza.

Simba haikuwa na wachezaji muhimu kwenye kikosi hicho ambao ni Mosses Phiri, Clatous Chama, Henock Inonga, Peter Banda, Mzamiru Yassin na Sadio Kanoute.

Kwa upande wa Kocha Msaidizi wa Dodoma Jiji, Kassim Liogope, alisema wame-

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >